# Nipashe

Jumatatu Julai 5, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580632

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Waziri** Mkuu aeleza nia ya serikali kukuza, kuboresha ushirika

UKURASA 3



**Wafanyabiashara** Feri kuondolewa kupisha ujenzi wa soko la kisasa

UKURASA 3



**Fati kuanza mazoezi Barca**

UKURASA 21

# CHANJO CORONA BURE

• **Serikali** yaboresha mwongozo shuleni na vyuoni... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**ACHINJWA KWA KUMFUMA MAMA NA MWANAMUME**

JESHI la Polisi Mkoa wa Geita linashikilia watu watano kwa...

UKURASA WA 19

**MOI YALETA MATUMAINI WANAOPATWA KIHARUSI**

TAASISI ya Mifupa (MOI) imeanzisha utoaji wa huduma ya kuleta...

UKURASA WA 19

**CHONGOLO AWAONYA WANASIASA WAVURUGAJI**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo...




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akimkabidhi kadi ya bima ya afya mkulima wa tumbaku, Athanas Gabriel wa Kikundi cha Ushirika Urambo mkoani Tabora, ikiwa ni kadi ya mkopo kutoka Benki ya NMB kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Tabora. NMB imetoa Sh. bilioni 5 ikiwa ni mkopo wa bima ya afya unaotarajiwa kuwasaidia wakulima zaidi ya 300,000 walio kwenye mazao ya kimkakati. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Mtoto auawa kwa kuliwa na fisi akiwa jandoni

UKURASA 2



Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Katoliki Mwanza, Mhashamu Renatus Nkwande, akimvisha mitra Askofu Simon Chibuga Masondole, wakati akipata Daraja Takatifu la Uaskofu na kumsimika kuwa Askofu wa Jimbo Katoliki Bunda katika viwanja vya Kanisa Kuu la Bunda, mkoani Mara. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

RIPOTI MAALUM

## Usugu shida ya ajira

• **Bingwa** uchumi alia tegemeo sekta binafsi nalo linasuasua... *Endelea Uk. 7*




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **NABI ATOA SIRI USHINDI, AIONYA YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Ofisa Muuguzi Kitengo cha Watoto wanaohitaji Uangalizi Maalum (PICU) wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Daud Mapunda, akitoa elimu kwa wananchi waliofika kutembelea banda lao kwenye Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Sabasaba Barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Chanjo ya corona bure

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema kuwa imeshakamilisha mwongozo wa uingizaji wa chanjo ya ugonjwa wa corona nchini pamoja na utunzwaji wake na itaanza kutolewa bure kwa watakaohitaji.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema chanjo hiyo itaanza kutolewa kwa watakaohitaji kwa hiari na haitatumika kama sehemu ya kufanya biashara kwa wananchi wake.

"Kupitia mwongozo huu, taratibu zote za utoaji wa chanjo zimeainishwa na itatolewa tu kwa wale wenye uhitaji bila malipo na kwa hiari yao, ambaye ataona ahitaji basi ataacha," alisema Prof. Makubi.

Aliwataka wananchi kufanya maamuzi sahihi katika kuamua kupata chanjo hiyo, na serikali itatoa elimu sahihi katika utoaji wa chanjo hiyo.

Kadhalika, Prof. Makubi alisema serikali itaanza kutoa chanjo hiyo baada ya kujiridhisha na usalama wake.

"Ili tuanze kutoa chanjo hii kwa wananchi, tunahitaji muda wa miezi sita ili kujiridhisha na suala la chanjo kabla ya kuanza kuitumia ili kuhakikisha usalama wa chanjo hizo kwa wananchi, ndio maana tukasema tutatoa elimu ili mwananchi apate uelewa wa kutosha juu ya chanjo hiyo," alisema Prof. Makubi.

Alieleza kuwa lengo la kuwapo kwa chanjo hiyo pia ni kuwasaidia watu ambao watahitaji kupata kwa urahisi tofauti na ilivyo sasa.

"Unakuta wakati mwingine mtu anahitaji kusafiri kwenda nje ya nchi kwa ajili ya kufanya kazi kubwa ya kitaifa, lakini nchi anayokwenda masharti yao lazima uwe umechanjwa, hivyo ikiwapo nchini itakuwa rahisi kwetu," alisisitiza.

**KIWANDA KUJENGWA**

Vilevile, alisema serikali ipo kwenye mpango wa kujenga kiwanda cha kutengeneza chanjo mbalimbali ikiwamo ya ugonjwa wa corona.

"Hapa nchini pia sisi tunatengeneza chanjo nyingi kwa mfano zipo chanjo za wanyama, tumeshaanza kutengeneza wenyewe...sasa tunataka kujenga kiwanda kwa ajili ya chanjo za kujikinga na magonjwa mbalimbali ya binadamu ikiwamo corona." Alisema kuwa ujenzi wa kiwanda hicho unakadiliwa kutumia zaidi ya Sh. bilioni 80 hadi kukamilika kwake kwa mujibu wa upembuzi yakinifu uliofanyika.

# Mtoto auawa kwa kuliwa na fisi akiwa jandoni

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MTOTO wa kike mwenye umri wa miaka minane aliyekuwa amepelekwa jandoni (jina linahifadhia) kwa ajili ya kuchezwa unyago katika kijiji cha Kivukoni, Kata ya Chiwale wilayani Masasi, mkoani Mtwara, ameuawa kwa kuliwa na fisi wakati akiwa amelala na wenzake.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo wakati akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kivukoni, Kata ya Chiwale, Mohamed Kazibule, alisema tukio hilo limetokea juzi majira ya saa tano usiku wakati mtoto huyo akiwa jandoni amelala na wenzake zaidi ya 30 katika jando hilo lililokuwa nje kidogo na kijiji hicho.

Alisema fisi huyo alimtafuta mtoto huyo ambaye ni mwanafunzi wa darasa la pili Shule ya Msingi Kivukoni, baada ya kumkamata akiwa ndani ya jando hilo lililokuwa limejengwa kwa kutumia kuta za nyasi.

Kazibule alisema fisi huyo alifika kwa kunyemelea hadi lililopokuwa jando hilo kisha kutoa nyasi na kumkamata mtoto huyo na kukimbia naye porini na kumtafuna.

Alisema fisi huyo alimtafuna mtoto huyo na kubakiza baadhi ya viungo vikiwamo fuvu la kichwa, mguu wa kulia na utumbo, ambavyo viligunduliwa na wananchi wa kijiji baada ya kupata taarifa kuwa mtoto huyo alikuwa amekamatwa na fisi.

"Mabaki ya viungo vya mwili wa mtoto huyo ambaye ametafunwa na fisi ameviacha na sisi tumeviokota ni fuvu la kichwa ambalo kwa sehemu kubwa limetafunwa, mguu wa kulia pamoja na utumbo...ndani ya jando wakati fisi anamchukua mtoto huyu kulikuwa na wasichana wengine zaidi ya watoto 30 tukio hili limeleta taharuki kubwa hapa kijijini," alisema Kazibule.

Alisema baada ya uongozi wa serikali ya kijiji hicho kupata taarifa kati ya majira ya saa saba na saa nane usiku kutoka kwa msimamizi wa wasichana hao, kwamba kuna tukio la fisi kuvamia jando la watoto wa kike na kufanikiwa kumkamata mtoto mmoja, walianza juhudi za kumsaka. Kazibule alisema uongozi wa kijiji kwa kushirikiana na wananchi walifika katika jando hilo na kuanza kufuatia nyayo za fisi huyo na kufanikiwa kuokota viungo vya mwili wa mtoto huyo na kuvichukua hadi kijijini.

Kwa upande wake Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Maulidi Dadi, alisema hatua zilizochukuliwa na kijiji ni kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi Wilaya ya Masasi kuhusu tukio hilo na polisi walifika na kuchukua mabaki ya viungo hivyo ambavyo wameshavikabidhi kwa familia ya mtoto huyo.

Mmoja wa maofisa wa Jeshi la Polisi ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini kwa kuwa sio msemaji rasmi wa tukio hilo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa mabaki ya viungo vya mwili wa mtoto wameshakabidhi kwa familia.

Akizungumza kwa uchungu mama mzazi wa mtoto huyo ambaye hata hivyo, hakutaka kutaja jina lake alisema familia imepokea kwa masikitiko kifo cha mtoto wao na viungo hivyo wameshazika jana huku familia hiyo ikisikitishwa na jambo hilo.

Alisema mtoto wao alitakiwa kutoka jandoni na wenzake kati ya Jumamosi au Jumapili kwa ajili ya kufanyiwa sherehe kama utamaduni na mila unavyotaka.

Hata hivyo, juhudi za Nipashe kumpata Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Mark Njelwa, kuzungumzia tukio hilo, ziligonga mwamba baada ya simu yake kuita bila ya kupokelewa na hata alipotumiwa ujumbe mfupi wa maandishi haukujibiwa.

Baadhi ya wananchi wa kijiji hicho waliozungumza na gazeti hili, akiwamo Saidi Bakari, alisema kuwa kwa sasa wapo katika tahuruki kubwa na wanajipanga kuanza kumsaka fisi huyo kwa kutumia silaha za jadi.

## ...Mwongozo udhibiti maambukizi shuleni na vyuoni waboreshwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imefanyia maboresho ya Mwongozo wa Udhibiti wa Maambukizi ya Covid-19, katika shule, vyuo na taasisi za elimu, ili ukidhi mahitaji ya sasa ya kuwakinga wanafunzi na maambukizi ya virusi vya corona.

Aidha, imehimiza wakuu wa taasisi hizo kuhakikisha zinazingatia na kutekeleza mwongozo huo kikamilifu.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, alisema wasimamizi wote wanapaswa kuuzingatia mwongozo huo.

Alisema wakuu wa taasisi za shule pamoja na vyuo wanatakiwa kutekeleza ipasavyo ikiwamo kuweka vyombo vya kunawa mikono na maji tiririka ili wanafunzi wanawe na kuhimiza matumizi ya barakoa.

"Mwaka jana tulitoa mwongozo huu, inawezekana, matumizi ya vifaa hivi yalipungua au yalisitishwa kabisa, sasa tunaagiza miundombinu ya maji ya kunawa irudishwe na itumike kama kawaida, wanafunzi wawe na barakoa angalau mbili au tatu ambazo zitamwezesha kufua na kubadilisha.

"Vile vile tunaagiza wasimamizi hao wa taasisi za elimu zikiwamo shule na vyuo waimarishe mifumo ya maisha kwa kufanya ukaguzi na usafi wa mara kwa mara katika madarasa na mabweni. Pia wafanye ukaguzi wa afya za wanafunzi na kutoa taarifa haraka kwa vyombo vinavyohusika na kwa utaratibu usiotia hofu wanapoona mwanafunzi ana kiashiria cha kuugua corona," alisema.

Aidha, Prof. Makubi aliwataka viongozi wote wa mikoa na wilaya kuongeza kasi ya udhibiti na kuhakikisha barakoa zinavaliwa wakati wote watu wanapoingia kwenye taasisi za serikali.

Vilevile, aliwataka viongozi wa dini kuendelea kuelimisha waumini wao katika nyumba za ibada kuhusu kujikinga na ugonjwa huo na kufuata taratibu zote za kujikinga kwa mujibu wa miongozo ambayo imeshatolewa na serikali.

"Tangu ugonjwa huu umeingia tumeshatoa miongozo 16, ambayo inatakiwa kufuatwa kwa ajili ya kujikinga na corona... tunaomba kasi hii ya kujikinga dhidi ya ugonjwa huu iongezeke kwa viongozi wetu wa dini tunaomba watekeleze," alisema.

Kadhalika, aliwataka wananchi kufuata miongozo na taratibu za kujikinga na ugonjwa huo kwa kuepuka mikusanyiko isiyokuwa ya lazima, na kujiongoza wenyewe hasa kwa wale wanaotumia usafiri wa daladala.

"Elimu hii imeshatolewa sana, wananchi wajiongoze wenyewe usikubali kukaa kwenye mikusanyiko, lakini hata kwenye daladala usisubiri mpaka uambiwe usipande daladala iliyojaa watu, wewe mwenyewe ukishaona imejaa usipande, subiri nyingine."

HABARI KITAIFA

# Majaliwa aeleza nia ya serikali kukuza ushirika

**Na Faustine Feliciane,**
TABORA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali ina dhamira ya dhati ya kuimarisha vyama vya ushirika ili kuhakikisha wakulima wanapata tija na manufaa ya shughuli za uchumi zinazoendeshwa na vyama hivyo.

Aidha, alisema serikali inaangalia kwa karibu shughuli za ushirika kwa kuwa inafahamu umuhimu wake kwa maendeleo ya wana ushirika kwenye ukuaji wa uchumi.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Ushirika Duniani iliyoanza Juni 29 na kufikia kilele juzi, mkoani Tabora.

Alisema kuwa ushirika ni sekta muhimu yenye mchango mkubwa kwa taifa, ambayo inahusisha shughuli za uchumi ikiwamo kilimo, uvuvi, ufugaji na vyanja nyingine ambazo zote hutoa ajira na kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa.

Aliwataka viongozi na watendaji wa sekta ya ushirika kuhakikisha kuwa vyama vya ushirika vinaendeshwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu ikiwamo kuvisimamia kwa misingi ya uadilifu, ili kuondokana na changamoto zinazoharibu taswira ya ushirika.

"Lazima tuzilinde mali za ushirika, jukumu tulilonalo viongozi wa ushirika ni kusimamia mali za ushirika na kuheshimu dhamana tulizopewa na wanaushirika," alisema Waziri Mkuu.

Akizungumzia mfumo wa stakabadhi ghalani, alisema ni mkombozi kwa wakulima kwa kuwa mkulima anapata fursa ya kupata bei yenye ushindani kupitia minada ya ununuzi ambayo mara nyingi ni ngumu kuipata kwa walanguzi.

"Naitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuendeleza juhudi za kuelimisha kuhusu mfumo huu na kuhakikisha hata maeneo yenye changamoto na mfumo elimu itolewe ili wakulima waelewe manufaa ya mfumo huu."

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alisema serikali inafanya marekebisho ya sheria ya vyama vya ushirika nchini ili kuhakikisha kuwa mali na shughuli zote za vyama hivyo zinasimamiwa na wanachama wenyewe.

Alisema lengo la marekebisho ya sheria hiyo iliyotungwa mwaka 2013, ni kuhakikisha kwamba vyama vya ushirika vinajisimamia vyenyewe bila kuingiliwa na viongozi kutoka serikalini.

"Ushirika haulazimishwi kwa kuwa si mali ya serikali na kujiunga ni hiari hakuna mtu anayelazimishwa, mamlaka ya serikali katika ushirika yana mipaka yake," alisisitiza.

Prof. Mkenda na kuongeza kuwa hakuna kiongozi mwenye mamlaka ya kuviagiza vyama vya ushirika kutoa fedha katika akaunti zao kwa ajili ya matumizi yoyote.

Awali, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, alisema wanaunga mkono juhudi za kufufua viwanda ili kuongeza thamani za mazao yanayozalishwa na wakulima.

Alisema kwa kipindi cha mwaka jana tayari viwanda vitatu vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika vimeanza kufanya kazi akivitaja viwanda vinavyomilikiwa na KACU, Chato na Mbogwe jambo ambalo linasaidia kuongeza bei ya mazao na ushindani wa soko.

Naye Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC), Theresia Chitumbi, alisema kauli mbiu ya maadhimisho hayo ni "Ushirika tujijenge upya kwa ubora na tija" inalenga kuonyesha ustahimilivu wa vyama vya ushirika katika kusaidia na kutoa michango ya utu kwa jamii katika kipindi cha majanga mbalimbali kama mabadiliko ya tabia nchi, uharibifu wa mazingira na hali ya hewa.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akifunua kitambaa na Waziri wa Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi la ufunguzi wa nyumba ya daktari Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja katika ziara yake. **PICHA: IKULU**

# Achinjwa kwa kumfuma mama mzazi na mwanamume mwingine

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

JESHI la Polisi Mkoa wa Geita linawashikilia watu watano kwa tuhuma za mauaji ya kumchinja Budagala Vita (26), kwa kumcharanga kwa mapanga shingoni na kufariki dunia baada ya kumkuta mama yake mzazi akifanya mapenzi na mwanamume mwingine.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Henry Mwaibambe, alisema tukio hilo limetokea Juni 28, mwaka huu katika Kijiji cha Bokondo, Tarafa ya Butundwe, Wilaya ya Geita.

Kamanda Mwaibambe alisema, Budagala aliuawa kwa kukatwa na mapanga shingoni na watu wasiojulikana baada ya kumkuta mama yake mzazi akifanya mapenzi na mwanamume mwingine, wakati baba yake mzazi akiwa safarini mkoani Kagera.

Alisema kiini cha tukio hilo ni mgogoro wa kifamilia, baada ya baba wa marehemu, Vita Bupilipili, kusafiri kwenda kutafuta maisha Juni 26, mwaka huu na kumuacha mke wake pamoja na mtoto wake huyo.

Alisema Budagala alimkuta mama yake mzazi akifanya mapenzi na mwanamume mwingine nyumbani kwao na kusababisha mgogoro ndani ya familia hiyo.

Alisema baada ya tukio hilo, mama mzazi wa marehemu alikimbia na kutokomea kusikojulikana na anatafutwa na Jeshi la Polisi ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Kadhalika, polisi inawashikilia watu watano kwa ajili ya mahojiano kuhusiana na tukio hilo. Majina ya watuhumiwa wote yamehifadhiwa kwa ajili ya uchunguzi.

Kamanda aliwataka wananchi wa mkoa huo kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa kuripoti matukio yote ya uhalifu katika vyombo vya sheria.

"Kwa umoja wetu tunaweza kutokomeza uhalifu," alisema.

# W'biashara Feri sasa kuhamishwa

**Na Moshi Lusonzo**

SERIKALI inatarajia kuwahamisha kwa muda wafanyabiashara katika soko la samaki la kimataifa la Feri jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya kupisha kazi ya uboreshaji na ujengaji wa miundombinu ya kisasa.

Akizungumza na wadau wa sekta ya uvuvi baada ya kufanya ziara kwenye soko jana, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema ujenzi huo ambao utaanza mwezi ujao, unalenga kulifanya soko hilo kuwa bora zaidi katika uuzaji wa samaki katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Alisema mradi huo utaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 3, kati ya fedha hizo Sh. bilioni 1.7 zimetolewa na Benki ya Dunia.

Waziri Ndaki, alisema kazi ya uakarabati huo zitafanyika katika maeneo mawili ambayo ni kanda moja na mbili, ambazo wafanyabiashara wanafanya kazi katika mazingira magumu ya wazi.

"Tumeanza na kanda hizi mbili ambazo ni muhimu katika uzalishaji wa samaki, tunataka kuona kila bidhaa inayotoka hapa inakuwa na ubora wa kimataifa na hivyo kuongeza kipato kwa serikali," alisema.

Aliwaondoa wasiwasi wavuvi na wachuuzi kwamba hakuna atakayeathirika wakati wa ujenzi huo, kwani serikali haitawaondoa kabisa, na badala yake watahamishwa kwa muda kwenda sehemu zingine pembeni ya soko hilo.

Hakuna atakayeathirika katika zoezi hili, serikali inajua mpo hapa kwa ajili ya kutafuta kipato, tutachokifanya tutawapeleka kwa muda sehemu ya jirani ili mwendelee kuuza na kununua samaki," ameongeza kusema.

Hata hivyo, ametoa onyo kwa mkandarasi atakayepata kazi hiyo kukamilisha kazi ndani ya miezi saba kama ilivyoainishwa, kinyume chake hatakubali kuona kazi hiyo ikisuasua na kusababisha usumbufu kwa wafanyabiashara.

Mtaalamu wa ujenzi huo, Debora Sengusia, alisema mradi huo ambao utaanza Agosti mwaka huu baada ya kupatikana kwa mkandarasi, utakuwa shirikishi ili kuhakikisha kila mfanyabiashara wa soko hilo anatambulika na kupatiwa maeneo ya kufanyia kazi.

"Kama wataalamu tumejipanga kuhakikisha katika zoezi la kuhawamisha kwa muda na kisha kuwarudisha sehemu zao, hakuna atakayelalamika kwa kukosa eneo la kufanyia kazi," alisema Sengusia.

## WATUMIAJI WA HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA

# Lijue Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Anga (TCAA CCC)

Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Anga (Tanzania Civil Aviation Authority Consumer Consultative Council (TCAA CCC)) ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 50 cha Sheria ya Usafiri wa Anga Sura ya 80 (the Civil Aviation Act, Cap 80).

Pamoja na mambo mengine, taasisi hii imeanzishwa kwa lengo la kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za usafiri wa anga. na kushauri Serikali juu ya masuala mbalimbali yahusuyo mtumiaji na sekta ya usafiri wa anga kwa ujumla

Baraza linaongozwa na Wajumbe ambao huteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya uchukuzi. Wajumbe hao ndio wenye dhamana ya kuandaa sera na kusimamia utekelezaji wa majukumu na malengo ya Baraza.

Kwa sasa Baraza liko chini ya Mwenyekiti wake Ndugu Shaaban Lidani Mtambalike, mbobezi wa masuala ya usafiri wa anga mwenye uzoefu wa zaidi ya miaka arobaini (40), utumishi wake ukianzia iliyokuwa Shirika la Ndege la Africa Mashariki (East African Airways) na kisha Shirika la Ndege la Taifa (Air Tanzania).


Aidha, shughuli za kila siku za Baraza zinaratibiwa na Sekretarieti inayoongozwa na Katibu Mtendaji ambaye anashirikiana na watumishi wengine kutekeleza mipango mbalimbali iliyowekwa na Wajumbe wa Baraza.

Kwa sasa, Katibu Mtendaji wa Baraza ni Ndugu Innocent Kyara, wakili wa mahakama kuu na mbobezi wa masuala ya utawala bora na kulinda na kutetea haki za watumiaji.

Baraza lilizinduliwa rasmi mnamo mwaka 2004 ambapo mwaka 2006 aliajiriwa Katibu Mtendaji wa Baraza wa Kwanza Ndugu Hamza Johari ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA).

Tangu wakati huo kumekuwepo na mafanikio kadhaa, mengi yakitokana na uwepo wa Mpango Mkakati ulioainisha maeneo ya vipaumbele ya kufanyiwa kazi. Mpango Mkakati huo unamaliza utekelezaji wake Juni, 2021.

Miongoni mwa mafanikio ya utekelezaji wa Mpango Mkakati 2015/16 - 2020/21 ni kama ifuatavyo;



*Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Usafiri wa Anga (TCAA-CCC), Innocent Kyara*

Elimu kwa umma

Katika kuelimisha umma juu ya majukumu ya Baraza, tumetengeneza Mpango wa Mawasiliano unaosaidia katika kuboresha mawasiliano baina ya Baraza na Wadau wake.

Tumekua tukitoa elimu kwa umma kwa kutumia tovuti yetu, mitandao ya kijamii, kushiriki katika maonesho ya wazi kama Sabasaba na Nanenane, kuandaa vipindi mbalimbali katika vyombo vya habari, kuendesha warsha kwa wadau na kuandaa program za mafunzo ya huduma kwa wateja katika viwanja vya ndege.

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza limefanikiwa kufikia wadau 12,017 sawa na 114% ya wadau 10,500 waliokusudiwa.

Kupokea na kushughulikia malalamiko ya watumiaji

Baraza hupokea na kushughulikia malalamiko mbalimbali ya wasafiri na watumiaji wa huduma za usafiri wa anga kwa ujumla.

Malalamiko hayo hushughulikiwa kwa mujibu wa utaratibu na mfumo wa malalamiko uliowekwa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA).

Kwa kipindi kinachoishia Juni 2021 tumepokea malalamiko 101 kupitia njia za maandishi na malalamiko 658 kupitia simu hivyo kutengeneza jumla ya malalamiko 767. Aidha, malalamiko hayo yote yaliweza kusikilizwa na kufungwa kwa wakati.

Malalamiko mengi yaliyopokelewa na kushughulikiwa na Baraza yanahusisha kuhairishwa mara kwa mara kwa safari za ndege, upotevu na uharibifu wa mizigo ya abiria, kutopata taarifa hasa pale inapotokea mabadiliko ya safari na maombi ya kurejeshewa fedha kufuatia kusitishwa kwa safari baada ya kufungwa kwa anga katika baadhi ya nchi kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Virusi vya Homa ya Uviko (Covid19).

Katika kipindi kijacho, Baraza limepanga kutengeneza mfumo wa kielekroniki wa kupokea malalamiko ambapo mtumiaji wa usafiri wa anga ataweza kuwasilisha malalamiko yake kwa njia rahisi ikiwemo njia ya simu kiganjani mwake kupitia APP maalumu.

Tangu kuanza kwa shughuli za Baraza mwaka 2004, mwitikio wa watu kutoa malalamiko bado ni mdogo jambo linaloonesha wengi ama hawafahamu haki zao au hawafahamu mahali pa kupeleka malalamiko yao.

Baraza limejipanga kukabiliana na changamoto hii kwa kuendelea kutoa elimu kwa umma kupitia njia mbalimbali za mawasiliano kwa umma.

Kuboresha ushirikiano wa kitaifa na kikanda katika masuala ya kulinda haki za watumiaji usafiri wa anga

Baraza limeendelea kushauriana na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi juu ya namna bora ya kutetea haki na maslahi ya watumiaji. Lengo kubwa ni kuongeza uzoefu katika taratibu mbalimbali za kumlinda na kumtetea mtumiaji.

Katika mikutano hiyo Baraza limekuwa likitoa mada na misimamo mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha maslahi ya mtumiaji yanazingatiwa.

Mikutano ambayo Baraza limeshiriki na kuwasilisha mada ni pamoja na Mikutano ya Kamati ya Uwezeshaji wa Usafiri wa Anga ya Afrika Mashariki, Mkutano wa Afrika wa Mamlaka za Udhibiti wa Huduma Mbalimbali (AFUR) na Mijadala ya Afrika juu ya kulinda watumiaji (African dialogue for Consumer Protection).

Aidha, Baraza limekuwa likishirikiana kwa ukaribu sana na Jukwaa la Watumiaji Tanzania (Tanzania Consumer Forum).

Jukwa hili ni mkusanyiko wa taasisi za Serikali zilizoanzishwa kwa Sheria za Bunge zinazotetea haki na maslahi ya mtumiaji wa huduma za bidhaa zinazodhibitiwa na zisizodhibitiwa.

Taasis hizi chini ya mwamvuli wa Jukwaa zimekua zikishirikiana kwa pamoja katika kuandaa shughuli mbalimbali za utetezi na elimu kwa mtumiaji. Shughuli hizo ni pamoja na maadhimisho ya Siku ya Mtumiaji Duniani na uchapishaji wa jarida la Sauti ya Mtumiaji linalotoka kila baada ya miezi mitatu.

Kushauri Serikali juu ya uboreshaji wa miundombinu ya Usafiri wa Anga

Katika hatua nyingine, Baraza limekua likitembelea viwanja mbalimbali vya ndege hapa nchini kwa lengo la kuangalia huduma mbalimbali zitolewazo katika viwanja vyetu kama zinafuata Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya usafiri wa anga. Ziara hizo pia zimelenga kubaini mapungufu na kushauriana na mamlaka husika jinsi ya kuboresha utoaji wa huduma katika viwanja vya ndege.

Tayari Baraza limetembelea Viwanja vya Ndege vya Songwe, Mwanza, Dodoma, Kigoma, Bukoba na mwezi Machi 2021 Baraza lilitembelea Kiwanja cha Ndege cha Geita ambapo mapungufu mbalimbali yalibainishwa na ushauri kutolewa kwa mamlaka husika.

Aidha katika robo ya kwanza ya mwa mwaka wa fedha 2021/2022 tumepanga kutembelea Jengo jipya la Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume, Zanzibar.pamoja na kuanza kutoa taarifa kila baada ya miezi mitatu juu ya masuala yahusuyo watumiaji nchini.

Taarifa hiyo itajikita na kuainisha gharama za tiketi ya ndege, muda wa safari za ndege (On-Time Performance) idadi ya malalamiko yaliyopokewa, idadi ya safari za ndege kuhairishwa (flight delays & cancellations) na matukio ya udokozi (pilferage) katika viwanja vya ndege.

Ni matarajio yetu kuwa taarifa hizi zitamsaidia mtumiaji katika kufanya maamuzi ya kutumia shirika la ndege lenye huduma bora zaidi. Aidha, taarifa hii itasaidia kuboresha huduma zitolewazo mashirika ya ndege.

Changamoto

Mwaka huu (2021/2021) umekuwa ni mwaka wenye changamoto kubwa na nyingi kwa watumiaji na usafiri wa anga kwa ujumla.

Itakumbukwa tarehe 17/03/2021, Baraza, wadau wa usafiri wa anga na wananchi wote wa Tanzania kwa ujumla tulikumbwa na simanzi kubwa kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hayati Dkt. John Pombe Magufuli ambaye mchango wake katika kuboresha sekta ya usafiri wa anga utaendelea kukumbukwa daima. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Katika hatua nyingine, tumeshuhudia mlipuko wa virusi vya homa ya uviko (Covid19) ukiathiri sekta ya usafiri wa anga ambapo nchi nyingi zilifunga anga lao hivyo watumiaji wengi kushindwa kusafiri.

Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, idadi ya abiria waliotumia usafiri wa anga ilipungua hadi kufikia watumiaji 2,495,379 ikilinganishwa na watumiaji 4,423,732 waliotumia usafiri wa anga katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20.

Pamoja na hayo, kukosekana kwa Sera na Sheria mahsusi ya kumlinda Mtumiaji (Consumer Protection Policy and Law) kumeendelea kuwa changamoto katika mapambano ya kutetea watumiaji wa huduma mbalimbali.

Matarajio

Katika hatua nyingine Baraza limekamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitano (2021/2022 - 2025/2026).

Utengenezaji wa Mkakati huu umezingatia na umelenga kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Awamu ya Tatu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26).

Mkakati umezingatia pia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) ambapo miongoni mwa vipaumbele vyake vitakavyotekelezwa na Baraza ni kulinda na kuimarisha misingi ya utu, usawa na haki, kukuza uchumi jumuishi na shindani na kuimarisha huduma na kulinda haki kwa makundi maalum.

Mkakati huu umelenga kuelimisha na kuongeza uelewa wa watumiaji wa usafiri wa anga juu ya haki na wajibu wao, kuongeza uelewa wa jamii kuhusu majukumu ya Baraza, kufuatilia na kushauri Serikali juu ya kutungwa kwa Sera na Sheria mahsusi ya kumlinda na kumtetea mtumiaji.

Mpango Mkakati huo unatarajiwa kuanza kutekelezwa kuanzia Julai 2021 ili kuweza kutimiza lengo lake kuu la kuwakilisha, kuelimisha, kutetea na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za Usafiri wa Anga mchini.

Mwisho, kuundwa kwa Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Anga (TCAA CCC) ni hatua madhubuti za Serikali katika utekelezaji wa Ibara ya 5.4 ya Sera ya Usafiri wa Anga ya Afrika (African Civil Aviation Policy (AFCAP)) inayoelekeza nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (African Union (AU)) kuratibu uanzishwaji wa Baraza la Watumiaji Usafiri wa Anga.

Kwa sasa Baraza linayo nambari ya simu (0800110190) ambayo wadau wetu wanaweza kupiga bure kwa ajili ya kuwasilisha maoni, ushauri au malalamiko mbalimbali katika usafiri wa anga.

Tunawakaribisha sana katika Ofisi za Baraza zilizoko katika majengo ya Wakala wa Ujenzi Tanzania (TBA) mkabala na Ubalozi wa Ufaransa, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Kinondoni, Dar es salaam.




*Watumishi wa Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Usafiri wa Anga (TCAA-CCC)wakitoa huduma kwa wageni mbalimbali waliotembelea banda lao.*

21634002

TOLEO MAALUM

WATUMIAJI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI

ewura CCC
Consumer Consultative Council

# EWURA CCC yawataka watumiaji kujua haki zao, kuzidai na kutimiza wajibu wao

*Na Mwandishi Wetu*

BARAZA la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA-CCC) limeundwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ya Mwaka 2001, Sura ya 414 na Kifungu cha 30, kwa lengo la kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA ambazo ni majisafi na usafi wa mazingira, umeme, gesi asilia na bidhaa zitokanazo na petroli.

Baraza hilo linaundwa na wajumbe wanaoteuliwa na Waziri anayehusika na Nishati, ambaye humteua Mwenyekiti na wajumbe kutoka kwenye orodha ya majina anayopewa baada ya mchakato wa usaili unaosimamiwa na wizara kukamilika.

Orodha hiyo inatoka kwenye jumuiya za wafanyabiashara au asasi inayotambuliwa kisheria, kama mwakilishi kutoka sekta binafsi. Makamu Mwenyekiti huchaguliwa na wajumbe wa Baraza kutoka kundi la wajumbe.

Majukumu makuu ya Baraza yanainishwa kwenye Sheria ya EWURA Kifungu cha 31(1); ambayo ni Kutetea na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA kwa kufanya maamuzi, kutoa maoni na taarifa pamoja na kushauriana na Mamlaka, Wizara na Mawaziri wa Sekta husika; Kupokea na kusambaza taarifa kuhusu maslahi ya watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA;

Mengine ni kuanzisha Kamati za watumiaji wa huduma za kimkoa pamoja na kushauriana nazo; na Kushauriana na wenye viwanda, Serikali na vikundi vingine vya watumiaji juu ya masuala yanayohusu watumiaji.

Kimsingi, EWURA CCC ni chombo cha kushauri (consultative body) na kutetea haki za watumiaji wa huduma za nishati na maji kwa kukuza ufahamu wa umma, kuendeleza uhusiano mzuri kikazi.

Ndani ya jukumu hilo, inawaleta pamoja watumiaji huduma washirikiane na mtandao wa watunga sera, watoa huduma, vyombo vya habari, mdhibiti, makundi ya watumia huduma, kamati za watumiaji na kuhamasisha majadiliano chanya miongoni mwa watendaji muhimu kati tasnia.

Katika kutekeleza majukumu yake, EWURA CCC inafanya kazi ikishirikiana na wadau mbalimbali kama vile Serikali, watoa huduma za nishati na maji, yaani TANESCO, mamlaka za maji na usafi wa mazingira na vituo vya mafuta.

Pia, kuna wauza gesi za majumbani, viongozi wa serikali za mitaa, viongozi wa dini na madhehebu, wenye viwanda, asasi za kiraia, vilevile taasisi za umma na binafsi.

Baraza linatekeleza dira yake kupitia mpango mkakati shirikishi



*Mhandisi Goodluck Mmari,*

ulioandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na yajayo katika utetezi na uwakilishi wa watumiaji nishati na maji.

Eneo jingine la majukumu, ni kutafiti na kushirikiana na Kamati za Watumiaji za kimikoa, watunga sera, watoa huduma, mdhibiti, vyombo vya habari na asasi nyinginezo za kimataifa za watumiaji wa huduma, ikilenga kukuza ufahamu wa sheria, sera na kanuni zinazohusu udhibiti wa nishati na maji.

**MALALAMIKO NA UTETEZI**

Hivi sasa EWURA CCC inasimama kuwa chombo kinachowaelimisha na kuwahamasisha watumiaji kulalamikia huduma duni wanapokutana nazo, kwa kuwa jambo hilo linapaswa kufanywa na watumiaji wenyewe.

Inaelezwa, kama mtumiaji hatolalamikia huduma mbovu ama duni, tafsiri yake ni kuwa mtumiaji huyu anachangia kuzorotesha ubora wa huduma na bidhaa zinazodhibitiwa na EWURA.

Baraza, pia katika kupokea malalamiko ya huduma zisizoridhisha, linaelekeza namna bora ya kuwasilisha malalamiko kwa watoa huduma, linatoa huduma za kisheria au uwakili kwa wahitaji wa huduma hizo, nyakati wa kusikiliza kesi.

Utaratibu wa kulalamika unamtaka mlalamikaji kuwasilisha malalamiko yake kwa maandishi kwa Mtoa Huduma asiporidhika na utatuzi, anapaswa kujaza fomu ya malalamiko ya EWURA na kuwasilisha malalamiko yake EWURA.

Inapotokea hajaridhika na utatuzi utakaofanywa na EWURA, mtumiaji anaweza kukata rufani kwenda Baraza la Ushindani na kwenye mchakato huo, jukumu la EWURA CCC ni kumsaidia mtumiaji ajue na kufuata utaratibu wa malalamiko na kupatiwa ufumbuzi.

**UTATUZI WA MALALAMIKO**

Akizungumzia utekelezaji wa baadhi ya malalamiko yanayojitokeza, Katibu Mtendaji EWURA CCC Mhandisi Goodluck Mmari, anatoa mfano wa mteja nyumba yake inapoungua kutokana na tatizo la umeme mkubwa.

Anasema, anachopaswa kufanya ni kutoa taarifa kwa mtoa huduma ambaye TANESCO, kwani ndiyo taasisi inayowajibika kuhakikisha umeme unaosambazwa, unakidhi viwango. Taarifa zake huwa zinapaswa kuwasilishwa kwa maandishi na anakabaki nayo mteja kwa ajili ya ufuatiliaji.

TANESCO nayo inawajibika kushughulikia kero iliyoripotiwa kwa mujibu wa Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa TANESCO.

**HAKI ZA WATUMIAJI**

Mmari anasema watumiaji wengi hawajui haki zao kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo ufuatiliaji na kujua tatizo. Anaendele: "Kuna matatizo mengine siyo ya kukimbilia polisi, bali ni kwenda kwenye taasisi husika na kudai haki yako katika taratibu zilizowekwa."

Mhandisi Mmari, pia anasisitiza kutumia na kutambua haki, kisha kuzidai pale inapotokea mtumiaji ulikuwa ukitimiza wajibu wake.

Anasema Baraza limekuwa likitumia njia mbalimbali kuhakikisha elimu ya mtumiaji inawafikia walengwa, mpaka wa ngazi ya chini kwa kutumia njia mbalimbali kama vile mitandao ya kijamii, kushiriki kwenye maonesho, kuwafuata wadau kwenye vikundi, semina kwa makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhudhuria kwenye vikao vinavyoitishwa na wenyeviti wa serikali za mitaa.

Pia, Baraza linafanya mikutano ya mwaka ambayo huwaleta pamoja wajumbe wa Baraza, Watumishi na Kamati za Watumiaji za mikoa kwa lengo la kujadili mafanikio, changamoto na kuweka mikakati ya kuongeza ufanisi wa kiutendaji kwa kipindi kijacho.

EWURA CCC imekuwa ikishiriki kwenye mikutano ya taftishi inayoandaliwa na kuitishwa na EWURA na kutoa maoni kupitia mikutano hiyo kuhusu masuala ya udhibiti, ikiwamo mabadiliko ya bei za huduma. Aidha, Baraza limekuwa likifanya mikutano ya uelimishaji kwa makundi mbalimbali ya wadau, ili kuwajengea uwezo wa kufahamu haki zao na wajibu na kuwahamasisha kuzidai pale zinapobinywa.

**CHANGAMOTO**

Hadi sasa Baraza linakumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo changamoto ya vyombo vya habari kukosa jicho la habari kwenye masual yanayohusu watumiaji wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa. Hali hii imeendelea kuyafanya masuala ya utetezi na udhibiti kuendelea kuonekana ni dhana ngeni. Changamoto nyingine ni watumiaji wengi kukosa utamaduni wa kusoma taarifa za huduma wanazotumia na namna ya kuzifahamu kiundani.

Toka kuanzishwa kwake, Baraza limefungua ofisi 16 katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Geita, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Mtwara, Singida, Tabora, Tanga, Rukwa na Ruvuma, lengo ni kuongeza ufanisi wa kiutendaji kwa kuwafikia wananchi katika maeneo wanayoishi.



*Katibu Mtendaji wa Baraza la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), Mhandisi Goodluck Mmari, akitoa ufafanuzi kwa washiriki kuhusu utaratibu unaotumiwa na Mamlaka za Maji nchini kuomba idhini ya kupandisha bei za huduma kwa Mdhibiti.*

216344102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF, TPLB umakini uongezwe mechi hizi za mwisho Ligi Kuu

**ZIMEBAKI** takribani raundi mbili kwa timu 15 kati ya 18 zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kuhitimisha msimu huu wa 2020/21, ambao utashuhudiwa zikishuka timu nne moja kwa moja Ligi Daraja la Kwanza.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Simba ipo kileleni ikiwa na pointi 73 zilizotokana na mechi 30, huku Yanga ikiwa nafasi ya pili na alama zake 70 baada ya kushuka dimbani mara 32 sawa na Azam FC yenye pointi 64 katika nafasi ya tatu.

Hata hivyo, mbio za kuwania ubingwa zinaonekana kubaki kwa farasi mmoja, Simba kutokana na kuhitaji pointi nne tu katika michezo yake minne iliyobaki ili kutwaa taji hilo kwa mara ya nne mfululizo.

Yanga hata ikishinda michezo zake zote mbili zilizosalia, itafikisha pointi 76 huku Azam FC, yenyewe kama ikishinda itamaliza na alama 70, hivyo ni vigumu kwa timu hizo kuwa na matumaini ya kutwaa ubingwa huo kwa msimu huu.

Kwa upande wa zinazoshuka daraja, tayari Mwadui FC imeaga mapema Ligi Kuu kutokana na kuvuna pointi 19 tu katika mechi 32, hivyo hata kama ikishinda michezo yake miwili iliyobaki itaishia kufikisha alama 25 ambazo ni chini ya Coastal Union (34), Gwambina FC (34) na Ihefu FC yenye alama 35, zote zikipigana vikumbo kukwepa kushuka daraja.

Lakini Ruvu Shooting yenye pointi 38, Mtibwa Sugar (38), Kagera Sugar (37), Mbeya City (36) na JKT Tanzania pointi 36, nazo hazipo sehemu salama kwani endapo zikipoteza michezo yao miwili iliyobaki huku Coastal Union, Gwambina, na Ihefu FC zikishinda, nazo zinaweza kujikuta zikiwa timu tatu kati ya zitakazoungana na Mwadui kushuka daraja.

Ikumbukwe pia timu mbili zilizoongoza Kundi A na B, kwenye Ligi Daraja la Kwanza zimepanda moja kwa moja Ligi Kuu, huku zilizomaliza nafasi ya ya pili katika makundi hayo mawili zikisubiri kucheza mechi za mtoano dhidi ya zitakazoshika nafasi ya 13 na 14 kwenye Ligi Kuu ili kuwania nafasi mbili za kucheza ligi hiyo ambayo msimu ujao itajumuisha timu 16 tu kutoka 18 za sasa.

Hivyo, ni wazi kwa namna msimamo wa Ligi Kuu ulivyo kwa sasa, huku timu zinazowania kubaki Ligi Kuu msimu ujao zikipishana kwa pointi chache, ushindani utakuwa mkubwa sana katika michezo hii miwili iliyobaki kwa kila timu.

Kwa mantiki hiyo, Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB), wanapaswa kuongeza umakini kwenye michezo iliyobaki ili kuepuka upangaji wa matokeo husuan kwa timu zinazowania kubaki Ligi Kuu pindi zitakapokutana na zile ambazo tayari zipo salama na hazina cha kupoteza.

Tunatambua pia hujuma na upangaji matokeo, mkono wa rushwa unaweza kupitia kwa waamuzi ambao kwa misimu kadhaa sasa wamekuwa wakilalamikiwa kwa kuzifinyanga sheria 17 za soka, hususan wakati kama huu wa kuelekea mwishoni mwa msimu.

Kwa kuzingatia hilo, tunaitaka TFF na TPLB kuongeza umakini ili kahakikisha timu zitakazoshuka daraja ama kubaki Ligi Kuu, ziwe zile zilizostahili kutokana na uwezo wao na si kwa kubebwa kwa njia yoyote ile.

Hilo halipaswi kuachwa kwa TFF na TPLB pekee, bali pia hawana budi kushirikisha TAKUKURU, lakini pia viongozi wa klabu, makocha pamoja na wachezaji wakiwa mstari wa mbele kukataa kuhusishwa kwa namna yoyote ile katika upangaji huo wa matokeo.

Nipashe tunataka kuona Ligi Kuu msimu ujao ushindani ukiongezeka na ligi yetu kuzidi kuwa bora zaidi barani Afrika, hilo linawezekana tu kama timu zote 16 shiriki zitatokana na uwezo wao binafsi kisoka na si kubebwa kwa namna yoyote ile.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Hongera Yanga, Simba sasa ijipange kwa Julai 25

**USHINDI** wa bao 1-0 ilioupata Yanga umeonekana kuleta faraja kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo ambao kwa muda mrefu walionekana kutokuwa na furaha kutokana na mwenendo wa timu yao.

Jumamosi, Yanga ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya watani wao wa jadi, Simba, ambao hata kama haitotwaa ubingwa na Ligi Kuu Tanzania Bara, tayari umewapa angalau faraja.

Kwa muda wa misimu miwili sasa ambayo Yanga imeonekana haina kikosi kizuri, imeweza kuifunga Simba mara mbili na kuisimamisha kwa sare mara mbili pia.

Msimu uliopita ilitoka nyuma kwa mabao 2-0 na kusawazisha yote, dakika 90 zikaisha kwa mabao 2-2 Januari 4, mwaka, kabla ya kuichapa bao 1-0 Mei 8, mwaka jana mwenye mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu.

Hali kadhalika, msimu huu baada ya sare ya bao 1-1 Novemba 7, mwaka jana, lakini ikiwa ni Ligi Kuu ya msimu huu, Yanga imeendelea kuonyesha umwamba kwa Simba Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Nitoe pongezi kwa viongozi, wanachama, benchi la ufundi la Yanga kwa kujipanga kisawasawa kuikabili Simba, timu ambayo hata wachezaji wenyewe wa mtaa wa Twiga na Jangwani wanasema ni nzuri na ngumu.

Licha ya kutokuwa na kikosi ghali na chenye uwezo mkubwa kama Simba, lakini Yanga chini ya kocha wao, Nasreddine Nabi imefanya kile ambacho wengi hawakukitarajia.

Kilichoonekana kwenye mechi hiyo ni kwamba Yanga ilicheza kimbinu zaidi dhidi ya watani zao, huku wenyewe wakicheza kwa mazoea zaidi.

Kilichoiponza Simba ni kwamba ilicheza kama vile inakwenda kucheza mechi zingine za kawaida za Ligi Kuu, au michuano mingine.

Pia Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes hakusoma alama za nyakati.

Wakati Yanga ikionekana kuifahamu zaidi Simba nguvu yake na udhaifu wake, wao hawakuonekana kuisoma Yanga, badala yake iliingia ndani kucheza vile vile inavyocheza siku zote ikawa imejaa kwenye mtego wa watani zao hao.

Ilicheza taratibu mno kipindi cha kwanza, wachezaji wakipoteza mipira bila sababu, wakionekana wazito, papara na pia kuonekana kama hawajiamini.

Hii iliwapa nafasi zaidi Yanga kufanya mashambulizi makali mfululizo hadi kupata bao la kuongoza.

Yanga ilipopata bao, mechi ikawa imeishia hapo. Gomes hakujua kuwa ilibidi Simba ianze kwa nguvu na kupata bao ili soka lichezwe.

Gomes hakujua kuwa siku zote Yanga huwa na wachezaji wazuri kwenye sanaa ya kujilinda, hivyo ikipata bao inakuwa ni ngumu mno kwa sababu wengi hurudi nyuma na kushambulia kwa kushtukiza.

Kama Simba ndiyo ingeanza kupata bao, mechi ingekuwa ya wazi kwa sababu timu hiyo haina falsafa ya kujilinda, ila kushambulia zaidi.

Hata hivyo, kama nilivyosema awali kuwa Kocha Nabi alionekana kuisoma zaidi Simba, hivyo pamoja na kushambulia kwa dakika 79, lakini haikuweza kupata bao.

Mara nyingi wachezaji wa Simba hufunga mabao yao ndani ya eneo la 18, hivyo mabeki wa Yanga na viungo wakijazana na kuwapa tabu sana mastraika wa Simba ambao walishindwa kubadilika.

Angalau, Rally Bwalya na Chris Mugalu walipiga mashuti nje ya eneo la hatari ni nusura wafunge, lakini kwa bahati mbaya wote wawili walikuwa wameingia kipindi cha pili, muda ambao ulikuwa na presha zaidi.

Simba ilihitaji wachezaji wapiga mashuti nje ya eneo la hatari kwa sababu plani zote mbili za kupenya ukuta kati na krosi zilikuwa zimeshindikana kutokana wingi wa wachezaji wa Yanga nyuma.

Kama tangu kipindi cha kwanza wangekuwa wanafanya hivyo, wangeweza kupata angalau sare, kama si kushinda.

Mechi imeisha, Simba inabidi kukubali matokeo na kwenda kwenye mechi nyingine ngumu kwao ya fainali ya Kombe la FA katika Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma Julai 25.

Nasema ni ngumu kwao kwa sababu kama imefungwa kwenye uwanja ambao unawabeba kwa falsafa yao ya mpira wa chini na pasi fupi fupi na sasa wanakwenda kwenye uwanja ambao si rafiki kwa aina yake ya mchezo, ni lazima itakuwa ngumu.

Kwa mpira uliochezwa Jumamosi iliyopita, Yanga ilistahili ushindi kutokana na kucheza kwa malengo, nidhamu na mbinu.

Simba nayo inabidi ijitafakari ione ilikosea wapi ili mechi ijayo iingie na mbinu ambazo itaona inafaa. Nitarajie pia utakuwa mchezo mzuri kwa sababu ni fainali na kuna kombe uwanjani.

RIPOTI MAALUM

## USUGU SHIDA YA AJIRA

# Bingwa uchumi alia tegemeo sekta binafsi nalo linasuasua

**Na Sanula Athanas**

UHABA wa ajira ni tatizo duniani kote, Tanzania ikiwa ni sehemu ya familia hiyo ingawa uainishaji wake unaweza kutofautiana kati ya taifa moja na lingine.

Kusimulia ushuhuda wa nchini, suala hilo liliibuka katika Mkutano wa Bunge la Bajeti uliomalizika wiki iliyopita jijini Dodoma, wabunge wakianika kinachowasibu vijana waliokwenda darasani na kuhitimu masomo yao, lakini fursa za ajira wanaambulia patupu.

Ikirejewa uhalisia uliopo, kinachojiri hakipishani sana na nadharia ya 'kupenya kwenye tundu la sindano'.

Kwa namna gani? Katika mkutano huo wa Bunge, serikali ilitangaza nafasi za ajira 9,675 kwa walimu na wataalamu wa afya mwezi uliopita.

Siku tano kabla ya kufungwa kwa dirisha la maombi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alibainisha takwimu za 'songombingo' la waombaji waliowafikia 120,000.

Baada ya dirisha la maombi kufungwa, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Profesa Riziki Shemdoe, alitangaza kupokea jumla ya maombi 137,020.

Katika mchanganuo wake, Profesa Shemdoe alibainisha kada ya ualimu ilivutia waombaji 99,583 na kada ya afya ilikuwa na waombaji 37,437, wakiwamo wenye ulemavu 1,099.

Uhalisia linganishi ni sawa na waombaji wanane tu ndiyo wanaopenya kwenye tundu la sindano kutoka katika kila kundi la wahitaji 100.

Hiyo inatosha kuhalalisha ujumbe unaotangazwa kwamba 'uhaba wa ajira ni tatizo nchini'.

Kimantiki, ni hoja inayobeba sura kuu mbili; upande mmoja ni mwongozo wa kinadharia na upande wa pili ni uzoefu wa kinachotokea, japo kwa kiasi kikubwa yote yanaangukia katika majawabu yaliyo sawa.

Wataalamu wa mipango ya uchumi wanaweka wazi kwamba uhaba wa ajira nchini unazalishwa katika uwiano usio sawa kati ya kasi ya kukua kwa uchumi na idadi ya wahitaji wa ajira, kwa maana ukuaji wa uchumi unapaswa kuzalisha fursa za ajira kuutumikia.

Katika hilo, Mkuu wa Kitengo cha Hazina cha Benki ya Biashara Kenya (KCB) Tawi la Tanzania, Pascal Machango, anashauri nchi iwezeshe vijana kiuchumi kwa kuwapatia mafunzo na mitaji ya biashara, ili wamudu kukabiliana na magumu ya uhaba wa ajira dhidi yao.

Machango anasema kwa sasa



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Tawi la Dar es Salaam, Profesa wa Uchumi, Honest Ngowi

kunashuhudiwa ongezeko kubwa la idadi ya watu nchini lisiloendana na fursa za ajira zilizopo.

"Fursa pekee ni kujikita katika mafunzo ya ufundi stadi na ujasiriamali ili vijana waweze kujiajiri na kuajiri wenzao," anashauri.

**PROFESA WA UCHUMI**

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Tawi la Dar es Salaam, Profesa wa Uchumi, Honest Ngowi, anakubaliana na hoja ya hali mbaya ya ajira nchini.

Nini kifanyike? Mchumi huyo anaishauri serikali ipitie sera, sheria na mikakati yake.

Anasema zamani serikali ilimudu kutoa ajira nyingi, lakini kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, ajira nyingi sasa zimehamia kwenye sekta binafsi.

"Kwa kutambua hilo, serikali iweke mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kushiriki katika shughuli za uchumi na uwekezaji, hilo litarahisisha fursa za ajira kwa Watanzania," anashauri.

Profesa Ngowi pia anashauri mitaala ya elimu sasa imulikwe kuwaandaa wahitimu wanaoendana na mahitaji ya soko la ajira.

"Wanafunzi waandaliwe na kupewa ujuzi ambao utawawezesha kujiajiri na kuajiri wenzao baada ya masomo.

"Wakati hayo yakifanyika, serikali iziangalie sera, mikakati na sheria zake ili kuboresha mazingira ya kuanzisha miradi ya uwekezaji na kiuchumi itakayotoa ajira kwa Watanzania," anashauri.

Taarifa ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) kuhusu Mwelekeo wa Ajira kwa Vijana Duniani ya mwaka jana, inaonesha tatizo la ajira kwa vijana wenye elimu kuanzia sekondari na kuendelea nchini ni kubwa zaidi kuliko wenye elimu chini yao.

"Kuwahimiza vijana wa kike na kiume kuhakikisha wanapata elimu ya juu si suluhisho la tatizo. Ni muhimu vyuo vikuu kuwa na mtaala unaozalisha wahitimu wenye ujuzi na wanaokidhi vigezo vilivyoko kwenye soko la ajira," ILO inatoa angalizo katika taarifa yake hiyo.

Shirika hilo linafafanua kuwa katika miaka ya karibuni, kumeshuhudiwa ongezeko kubwa la wahitimu wa vyuo vikuu, huku waajiri wakihitaji idadi ndogo ya nguvu kazi ya wahitimu hao, hivyo wengi wao kukosa ajira.

Katika hoja hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan, alipozungumza na vijana jijini Mwanza Juni 15, mwaka huu, aliweka wazi kuwapo upungufu mkubwa wa vijana walioko kwenye ajira, ilhali uwezekano wa kuongezeka bado uko gizani.

Kwa mujibu wa Rais Samia, hadi sasa Tanzania kuna jumla ya vijana milioni 20.7 wenye umri kati ya miaka 15 na 35, lakini ndani ya kundi hilo, asilimia 11.4 ya wenye sifa za kuajiriwa, hawako kazini.

Rais Samia katika ufafanuzi wake, anaangukia kwenye alilolitamka Profesa Ngowi, kwamba fursa za ajira serikalini ni finyu na mtazamo mpana uko sekta binafsi.

Serikali iliyoko madarakani, imeahidi kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025, kwamba itatengeneza ajira mpya milioni nane katika kipindi hicho cha miaka mitano.

**HALI ILIVYO NCHINI**

Sekretarieti ya Ajira ilitoa taarifa Desemba 17, 2018 inayobainisha kuwapo jumla ya maombi ya ajira serikalini 594,300 kati ya Novemba 2015 na Desemba 2018, lakini waliopata kazi hizo ni watu 6,554.

Ni katika kipindi hicho, serikali ilikuwa imetangaza kusitisha kwa muda kutoa ajira mpya serikalini na kupandishwa vyeo watumishi wa umma (isipokuwa kwa kada nyeti), ili kupisha uhakiki wa watumishi hewa na wenye vyeti vya kughushi.

Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) iliripoti Agosti 14, 2019 kuwa kiwango cha ajira kilipungua kwenye sekta binafsi kutoka waajiriwa 239,019 mwaka 2016/17 hadi ajira 137,054 mwaka uliofuata, yaani 2017/18.

**CHIMBUKO NA HISTORIA**

Kwa Tanzania, uhaba wa ajira ni historia iliyokuwapo kwa muda mrefu, viongozi mbalimbali wa kitaifa katika awamu zao, kila mmoja kwa namna yake ana simulizi jinsi tatizo hilo lilivyomtesa.

Tangu alipochukua uongozi wa nchi mwaka 1961, Rais Julius Nyerere aliweka mipango ya uchumi iliyokuwa na mtindo wa uwekezaji uliotafsiri kukuza uchumi wa nchi ulioendana na kutanua fursa za ajira.

Historia inarejea alianza safari ya uongozi wa nchi kwa kutekeleza mpango wa maendeleo wa muda mfupi (1961-1964).

Maudhui ya mpango huo yaligusa kufungua nyanja zote za kisekta zilizofungwa na ukoloni, elimu kwa wote ikibeba nafasi ya kipekee, pia kilimo ambacho daima Mwalimu Nyerere na historia ya nchi haijawahi kukinyima kipaumbele, kikiwa ni mwajiri mkuu wa wananchi kabla na baada ya uhuru.

Mikakati yenye dira kuu ilianza rasmi mwaka 1964, ambao umebeba historia kubwa katika uamuzi wenye sura nyingi kitaifa.

Mojawapo ni Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (1964-1969), ambao nao haukusahau uwekezaji wa kimkakati kwa mwajiri mkuu, yaani Sekta ya Kilimo.

Mpango huo pia ulizama kwa mshirika mkuu wa kilimo na mwajiri namba mbili, yaani Sekta ya Viwanda, serikali ikijenga viwanda kwa wingi.

Uongozi wa Mwalimu Nyerere ulipambana kufanikisha alichokiita 'tuondokane na kuzalisha tusichokitumia na kutumia tusichozalisha, kuhamia kwenye kuzalisha tunachokitumia'.

Utekelezaji wake ndiyo uliibua ushuhuda wa kufunguliwa kwa viwanda vingi vya nguo kama vile Mutex (Mara), Mwatex (Mwanza) na Urafiki (Dar es Salaam), dhana iliyoongeza kasi ya uzalishaji pamba mashambani na kwa namna ya pekee kunyanyua uchumi wa Kanda ya Ziwa.

Vivyo hivyo, mlolongo wa viwanda mbali na vya nguo, uliendana na kufunguliwa kampuni lukuki za kibiashara nchini kuhudumia mahitaji ya viwanda na kilimo.

Hapo ndipo panaposhuhudiwa mathalani Shirika la Biashara la Taifa (STC), kampuni za biashara za mikoa na za maeneo maalum kama vile HOSCO - wauzaji wa vifaa vya nyumbani na BHESCO waliouza vifaa vya umeme na ujenzi.

Vilevile, Sekta ya Viwanda ilitanuliwa kwa namna ya kufunguliwa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) ambalo liliwekewa mfumo wa kitaifa uliomfikia kila Mtanzania aliko, akiwamo mkulima, kupitia tawi la ofisi za mikoa zilizopo hadi sasa.

Ujumla wa tafsiri inayopatikana hapo, ni kufunguliwa milango mingi ya ajira kwa Watanzania wa kada zote.

Kiuchumi, hiyo ikafanya uwapo wa shughuli nyingi za fani mbalimbali ambazo kitaalamu zinazaa kinachoitwa 'multiplier effect', kwamba jambo moja linakuza shughuli zingine za kiuchumi, ambazo ndani yake zinafungua fursa za ajira. Ndicho kilichotokea.

Ni faida mojawapo ya mipango hiyo ya uchumi katika zama za Mwalimu Nyerere, ambayo iliitekelezwa kwa awamu tatu, japo haikufika tamati ya dira yake kutokana na Tanzania kuingia mfumo huria mwaka 1985 ilhali mipango yenyewe ilikuwa kwenye mfumo hodhi kiuchumi.

Huo ni msimu unaobeba alama kubwa katika historia ya Tanzania, kwamba ni mwaka mmoja tangu kustaafu kwa mwasisi wa taifa, Mwalimu Nyerere, aliyetumikia uongozi kwa miaka 24 sambamba na kukoma kwa miaka 21 ya mfumo hodhi wa kisiasa na kiuchumi kitaifa.

***Usikose kesho namna Mzee Rukhsa na mrithi wake, Hayati Benjamin Mkapa, walivyopokea kijiti cha uongozi na kuendeleza 'biashara' ya ajira kwa Watanzania, kila mmoja katika zama zake za miaka 10.**

# W'biashara waondolewa urasimu uagizaji mbolea

**Na Rose Jacob,** MWANZA

KUTOKANA na kupanda kwa bei ya mbolea nchini na kusababisha adha kwa wakulima, serikali imetangaza kuruhusu uingizaji wa mbolea kwa kampuni bila kutumia zabuni kuhakikisha sekta ya kilimo haiathiriki.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adlof Mkenda, alisema kutokana na kuwapo kwa Covid- 19, baadhi ya viwanda vimepuuza uzalishaji na kusababisha bei ya mbolea kupanda, kutokana na mahitaji makubwa yasiyoendana na upatikanaji.

Alisema mahitaji ya mbolea kwa msimu 2020/2021 yalifikia tani 718.052 na upatikanaji ulifikia asilimia 82 hadi Mei 2021.

"Upatikanaji wa mbolea nchini unategemea uzalishaji unaofanywa na viwanda vya ndani, upungufu hufidiwa kwa kuagiza nje kwa kutumia mfumo wa pamoja wa manunuzi na uingizaji unafanywa na kampuni za mbolea zilizopatiwa vibali na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania(TFRA)," alisema Mkenda.

Aidha, Mkenda alisema katika mazingira ya kawaida, kipindi cha Julai na Oktoba kila mwaka watumiaji wakubwa wa mbolea duniani hupunguza bei katika soko la dunia, lakini mwaka 2021 hali imekuwa tofauti bei imependa kutokana na sababu mbalimbali.

Aidha Mkenda alisema kwa kuzingatia kanuni ya 7(4) ya kanuni za ununuzi wa mbolea kwa pamoja na 49 za mwaka 2017, hivyo wafanyabiashara wa mbolea wote wenye nia wa kuingiza pembejeo nchini, wako huru bila kupitia zabuni ya uingizaji wa mbolea kwa pamoja.

"Mfumo wa Manunuzi ya pamoja hauwezi kukidhi mahitaji ya utoaji wa mbolea, Wizara ya Kilimo imeamua kuruhusu ushindani, ili kila mwenye uwezo wa kuleta pembejeo na kuuza, hivyo kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha upatikanaji wa mbolea kwa matumizi ya ndani na nchi jirani," alisema Mkenda.




Afisa Mkuu wa Masoko na Uhusiano wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS, Martha Mashiku, akitoa maelezo kuhusu fursa zilizopo katika mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja kwa mwananchi aliyefika katika banda la kampuni hiyo kwenye Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere Barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Vitambulisho vyakosesha matibabu maelfu ya wazee

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZEE 29,916 kati ya 32,568 wa Mkoa wa Njombe wanajigharamia matibabu kwa sababu ya kukosa vitambulisho vya kuwawezesha kupata huduma hiyo bure katika hospitali za serikali.

Wazee 2,652 pekee ndio wanaotajwa kuwa na vitambulisho hivyo.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Njombe, Telesia Yomo, katika kikao kazi cha kujadili hali ya walemavu na wazee kupitia changamoto wanazokabiliwa nazo ambapo taarifa zinaeleza kuwapo kwa wazee 2,652 pekee wenye vitambulisho, hivyo kati ya wazee 32,568 waliopo mkoani humo.

"Njombe DC wapo 5,952, TC wanao 7,583, Wanging'ombe wako 872. Idadi hizi zinatusaidia kujua ni kwa kiasi gani na kiwango gani tunaweza kuwaandalia huduma za matibabu," alisema Yomo.

Mmoja wa wadau, Dk. Saleh Abdalah kutoka Kituo cha wenye ulemavu cha Inuka Wanging'ombe ameiomba serikali kuongeza nguvu ya kuwasaidia wazee pamoja na wenye ulemavu.

"Wazee kwanza hii ni concept (dhana) ambayo ipo kwanye Ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020, kwa hiyo sio hiari, ni lazima... kwa hiyo ni vizuri tukawa tunawatengenezea makundi na tukawalipia huduma ya matibabu kwenye mifuko maalum," alisema Dk. Abdalah.

Pamoja na jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na wadau hao, likiwamo Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kusini Njombe kuwajengea wazee kituo cha kuwalelea huko Kibena, lakini mlezi wa kituo hicho, Tumain Mbangala, alisema wazee wengi wamekuwa wakigoma kuishi hapo licha ya huduma zote muhimu kupatikana.

Mwenyekiti wa Wazee Halmashauri ya Mji Njombe, Bhokela Zacharia, alisema kuwa endapo serikali itakwenda na kasi ya sasa katika kuyasaidia makundi hayo, wanaamini wataepukana na changamoto lukuki zinazowakabili.

"Zamani tulikuwa tunakumbwa na changamoto ya kutopokelewa vizuri sisi kama wazee, tunanyanyapaliwa, lakini kwa mwanzo huu nadhani tutafanikiwa," alisema Zacharia.

Takwimu zinaonyesha kuwapo kwa wenye ulemavu 2,686 wa aina tofauti ikiwamo wa viungo, kutoona, wasiosikia na ulemavu wa ngozi mkoani Njombe, huku watoto wenye ulemavu chini ya miaka mitano wakiwa 76.

# EWURA yaongezewa uwezo wa kutambua vinasaba kwenye mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limekabidhi maabara mbili zinazotembea na mashine mbili kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) kwa ajili ya kutambua vinasaba kwenye mafuta yanayouzwa katika soko la ndani, hasa kwenye vituo vya mafuta.

Hafla ya makabidhiano ya maabara hizo ilifanyika jijini Dar es Salaam na kushuhudiwa na maofisa wa TBS na EWURA.

Mkuu wa Shughuli za Uwekaji Vinasaba wa TBS, Mhandisi Frolian Batakanwa, alisema maabara hizo pamoja na mashine mbili zitafanyakazi na kama ikitokea mashine mmoja ikaharibika, nyingine itafanyakazi ili kuhakikisha kazi inafanyika kwa ufasaha zaidi.

Alisema shirika hilo lilianza utaratibu wa kutambua kiasi cha vinasaba kwenye mafuta hasa kwenye soko la ndani pale TBS ilipoanza kuweka vinasaba kwenye mafuta, hivyo hatua hiyo ni mwendelezo wa kuipatia EWURA vifaa ambavyo itavitumia kwenye kazi zake.

"Kwa hiyo kwenye masoko nchini tuna magari yenye maabara kwa ajili ya kutambua vinasaba na hiyo itatusaidia kujua mafuta ambayo hayakidhi ubora au yamechanganywa na mafuta mengine," alifafanua Batakanwa.

Kwa mujibu wa Batakanwa, maabara hizo zinatembea na ndani kuna mashine kwa ajili ya kufanya utambuzi, kompyuta ya kuendesha mashine pamoja na vifaa vingine.

Kwa hatua hiyo, Batakanwa alisema Watanzania watarajie shughuli ya uwekaji vinasaba na kutambua kama vipo kwa usahihi kwenye mafuta itafanyika kwa ufasaha wa hali ya juu.

Kwa upande wake Meneja Ufundi wa EWURA, Mhandisi Shaban Seleman, alisema wao kama wasimamizi wa ubora wa mafuta yanayosambazwa nchini watatumia maabara hizo kuhakikisha mafuta yote yanayosambazwa nchini yanakidhi viwango vya ubora ili kutoharibu magari na mitambo mingine inayotumia mafuta.

# Waziri: Changamkieni hati ardhi kwa siku moja

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka wakazi wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani waliorasimishiwa makazi yao kutumia fursa ya Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa kujipatia hatimiliki za ardhi zinazopatikana ndani ya siku moja.

Akizungumza wakati wa kutembelea Banda la Wizara ya Ardhi katika maonyesho hayo mwishoni mwa wiki katika viwanja vya Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam, Mabula alisema maonyesho ya Sabasaba ni fursa nzuri kwa wananchi wa mikoa hiyo kujipatia hatimiliki za ardhi na huduma nyingine za sekta hiyo kwa uharaka zaidi.

Katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya mwaka huu Wizara inatoa hatimiliki za ardhi kwa wale wananchi waliorasimishiwa makazi yao na kuwa na nyaraka muhimu kupata hati ndani ya siku moja.

**TANGAZO**

# MINIMUM DISCLOSURE OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

NMB
Karibu yako

| S/N | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | **SAVINGS ACCOUNTS** | |
| | Required minimum opening balance | Business saving A/C TZS 100,000, USD 100,EUR 100,GBP 100; Bonus A/C TZS 50,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Mtoto A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Chipukizi A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Pamoja A/C TZS 30,000 |
| | Transaction fee | N/A |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | FREE |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 4,000 for amount up to TZS 5Million; TZS 4,000plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Withdrawal bulky without notice | OTC: TZS 4,000 for amount up to TZS 5Million; TZS 4,000plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Savings Card/Passbook | N/A |
| | Passbook/Card Replacement | TZS 11,800 |
| | Closing Account | TZS 9,440 USD 11.8, EUR 11.8 & GBP 11.8 |
| 2 | **CURRENT ACCOUNT** | |
| | Required minimum opening balance | Business, Supply Chain, Trade Business, Agribusiness Overdraft, Agribusiness Loans, Agri-General, Corporate, Emerging Corporate A/C - TZS 100,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Personal A/C - TZS 15,000; Mwanachuo & Chapchap A/C - TZS 10,000; Wisdom - FREE; Group A/C - TZS 30,000; Fanikiwa A/C - TZS 20,000; Exclusive A/C - TZS 1Million; Executive A/C - TZS 500,000; Kilimo & Bonus A/C - TZS 50,000; Float & Scheme Financing A/C - FREE; Notice Investment A/C - TZS 500Million;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- ZERO |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | Personal A/C - TZS 1,800; Business A/C & Agribusiness - TZS 15,340; Corporate, Insitution & Trade Business A/C - TZS 19,200; Exclusive A/C - TZS 35,400; Executive A/C - TZS 23,600; Emerging Corporate - TZS 19,200; Fanikiwa - TZS 2,000; Personal A/C Agribusiness - TZS 2,048; Kilimo is - TZS 1,800; for Forex A/C charges are Equivalent to TZS;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- FREE |
| | Transaction fee | N/A |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Bank Drafts | NA |
| | Bank Drafts cancellation charge | NA |
| | Cheque book (100 leaves) | TZS 48,380 USD 35.4, EUR 23.6 & GBP 17.7 |
| | Cash Withdrawal at Counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Special Clearance | TZS 53,100 USD 52.8, EUR 46 & GBP 39.5 |
| | Cheque withdraw over the counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Dishonoured cheque | 1.5% of the amount Min 64,000 Max TZS 118,000 |
| | Cash Payment to 3rd party | N/A |
| | Cash Deposit Charge | N/A |
| | Overdrawn account interest charge | N/A |
| | Unarranged Overdraft | N/A |
| | Bulk cash Deposit | FREE |
| | Bulk cash Withdrawal | N/A |
| | Stop Payment orders | TZS 35,400, USD 23.6, EUR 17.7 & GBP 17.7 |
| | Standing Orders ( within the same bank) | FREE |
| | Standing Orders ( to other bank) | TZS 19,710 |
| | Letter of introduction | N/A |
| | Salary handling | TZS 3,540 |
| | School fees deposits | FREE |
| | TRA collection | FREE |
| | Safe custody charges | N/A |
| | Safe custody access fees | N/A |
| 3 | **EFT** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | FREE |
| | To other Banks ( On Others) | 2000 |
| (b) | Outward Transfers | 2000 |
| | Inward Transfers | FREE |
| 4 | **TISS** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | N/A |
| | To other Banks ( On Others) | TZS 10,000 |
| (b) | Outward Transfers | TZS 10,000 |
| | Inward Transfers | FREE |

| 5 | **FOREIGN EXCHANGE ACCOUNT** | **Savings Acc** | **Current Acc** |
|---|---|---|---|
| | Transaction fee | N/A | N/A |
| | Statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | |
| | Interim statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | USD1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month |
| | Withdrawal Charges | 0.25% of the amount - forex | 0.25% of the amount - forex |
| | Cash Deposit Charge | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) |
| | Purchase/Sale of TC transactions over the counter | N/A | N/A |
| | Purchase of Foreign Cheque | N/A | N/A |
| | Sale/ Purchase of cash passport | N/A | N/A |
| | Telex/SWIFT | USD 58 | USD 58 |
| | Transfer from foreign currency denominated account to local account | N/A | N/A |
| | Outward foreign transfers | USD 58 | USD 58 |
| | Inward foreign transfers - Customers | FREE | FREE |
| 6 | **ATM CARD AND TRANSACTIONS RELATED** | | |
| (a) | Local Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | N/A |
| (b) | International Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - FREE; World Reward - FREE |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| (c) | ATM Withdrawals: | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | From TZS 1,100 - 1,500 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | TZS 3,540 |
| | ATM mini statement | N/A | TZS 413 |
| | Bill payments through ATM | N/A | FREE |
| (d) | POS | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | TZS 1,770 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | FREE |
| 7 | **MOBILE (SMS) BANKING** | | |
| | Balance Inquiry | N/A | TZS 400 |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers (within NMB) | N/A | FREE |
| 8 | **INTERNET BANKING** | | |
| (a) | Domestic: | | |
| | Balance Inquiry | FREE | FREE |
| | Payments | TZS 640 | TZS 640 |
| (b) | International | | |
| | Balance Inquiry | N/A | FREE |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers | N/A | USD 45 |
| 9 | **MONEY REMITTANCES** | | |
| (a) | Western Union | | |
| | Sending | N/A | N/A |
| | Received | N/A | N/A |
| (b) | Money Gram | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (c) | Coinstar | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (d) | Travelex | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (e) | Africash | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (f) | Others (Specify) | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |

| 10 | **BANKING SECTOR - DEPOSITS & LENDING RATES** | | |
|---|---|---|---|
| **A** | **TYPES OF LENDING RATES** | **LENDING RATES - PA (%)** | |
| | | **TZS** | **USD** |
| (a) | Flat | | |
| (b) | Declining | 17% | 9% |
| (c) | Negotiable | | |

**B** **FIXED DEPOSITS**

| PERIOD | TZS | | | USD | GBP |
|---|---|---|---|---|---|
| | 500K><9.9Mil | 10M><99.9M | 100M><199M | 2000-49,999 | 2000-49,999 |
| I Month | 2.00% | 2.25% | 2.50% | 0.45% | 0.25% |
| 2 Months | 2.50% | 2.75% | 3.00% | 0.55% | 0.30% |
| 3 Months | 3.00% | 3.25% | 3.50% | 0.70% | 0.40% |
| 6 Months | 3.50% | 4.00% | 4.50% | 0.80% | 0.50% |
| 9 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 12 Months | 5.00% | 6.00% | 7.00% | 1.00% | 0.60% |
| 13-24 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 25-36 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |

**Signed By:**

**Aloyse Maro**
**Head Retail Products & Channels**

**Filbert Mponzi**
**Chief Retail Banking**




www.nmbbank.co.tz

216343702

# TanTrade yapigwa jeki kuboresha Sabasaba

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) imeingia makubaliano maalum na Benki ya NBC yanayohusisha ufadhili wa benki hiyo katika ujenzi na ukarabati wa kumbi kubwa za kisasa kwenye Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba).

Maboresho hayo pia yanahusisha ujenzi wa sanamu ya Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli.

Wakizungumza wakati wa hafla ya kusaini hati ya makubaliano yenye thamani ya Sh. milioni 420 jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade, Balozi Mteule Edwin Rutageruka na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, walisema hatua hiyo inalenga kuleta mapinduzi makubwa kwenye maonesho hayo yanayoendelea, huku yakivutia maelfu ya washiriki kutoka ndani na nje ya nchi.

Balozi Mteule Rutagaruka alisema mkataba huo unahusisha kipindi cha miaka mitatu, huku akitaja maeneo yatakayoguswa na ufadhili wa benki hiyo kuwa ni pamoja na ukarabati mkubwa wa ukumbi unaofahamika kwa jina 'Sabasaba' wenye ukubwa wa mita za mraba 1,600 ili kuwa na hadhi ya juu zaidi si tu katika maonyesho hayo bali pia katika Wilaya yote ya Temeke.

"Kwa jitihada hizi za Benki ya NBC, kwa sasa ukumbi huu ambao pia unatumika kama banda la maonyesho ndio linalovutia zaidi washiriki wa kimataifa na limebeba hadhi hiyo ya kimataifa na ndipo yanapofanyika maonesho ya madini.

Zaidi pia linatumika kamba kumbi ya mikutano ya kisiasa na shughuli za kijamii zikiwamo harusi," alisema.

Alitaja kumbi nyingine zitakazohusishwa na ufadhili huo ni wa mikutano wa Rashid Mfaume Kawawa unaofanyiwa ukarabati mkubwa sambamba na ukarabati wa banda la bidhaa za viwanda vya Tanzania ambao utakarabatiwa katika hatua ya pili ya utekelezaji wa makubaliano hayo.

Kwa upande wake Sabi alisema ni heshima kubwa kwa benki hiyo kuingia katika ushirikiano huo kwa kuwa utatoa fursa kwao kufanikisha adhima ya msingi ya kuendelea kuwahudumia wadau wake muhimu wakiwemo wafanyabiashara wanaoshiriki maonyesho hayo.

Kuhusu ujenzi wa sanamu ya Hayati John Magufuli, Sabi alisema unalenga kukumbuka jitihada na mchango wake katika kuinua uchumi wa viwanda nchini, ambao ni kichocheo kikubwa cha biashara na ndio msingi wa maonyesho hayo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Balozi Mteule Edwin Rutageruka (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, wakisaini hati ya makubaliano inayohusisha ufadhili wa benki hiyo, katika ujenzi na ukarabati wa kumbi kubwa za kisasa kwenye Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam juzi. **PICHA: NA MPIGAPICHA WETU**

# W'biashara wanawake wamkubali Rais Samia

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), Mwajuma Hamza, amesema kauli iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni ya kuboresha mazingira ya uwekezaji pamoja na ya biashara nchini, imeanza kuleta matumaini kwa wanawake wanaojihusisha na ujasiriamali.

Mwajuma alitoa kauli hiyo jana katika banda la TWCC kwenye maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) yaliyoanza Juni 28, mwaka huu.

Alisema kauli hiyo ya Rais Samia ya kuboresha mazingira ya biashara, pia imechochea idadi kubwa ya wanawake wajasiriamali kujitokeza kwa wingi katika maonyesho hayo ambayo yanashirikisha watu kutoka ndani na nje ya Tanzania, kuonyesha na kutangaza bidhaa zao ikiwamo kujifunza fursa za kushindana katika soko la kimataifa.

"Kauli ya Rais Samia imeleta matumaini makubwa husani kwa wanawake wengi wafanyabiashara ambao walikuwa wamekata tamaa, walikuwa hawaoni mwanga, lakini kwa sasa naona kila mmoja anasema yuko tayari kufanya biashara na ndiyo maana mwaka huu hata katika maonyesho haya wamejaa hakuna hata nafasi iliyobaki katika mabanda yao, tofauti na miaka mingine iliyopita," alisema Mwajuma."

"Wanawake wamekuja na bidhaa bora za hali ya juu, watu wanaopita humu kwenye mabanda yao wanashangaa sana kutokana na bidhaa hizo wanazozikuta humu, kwa kweli ni jambo la kumpongeza sana Rais wetu."

"Kwa hiyo wajasiriamali hawa wanawake, wana imani na serikali ya Rais Samia, katika siku hizi 100 tangu aingie madarakani tumemwelewa sana na tunamkaribisha sana akija kwenye maonyesho haya, aje kututembelea na sisi wanawake katika banda letu ili tumweleze namna alivyotufurahisha, hatuna cha kumlipa ila tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu," alisema Mwajuma.

## 'Onyo kutumia bidhaa zisizokidhi viwango'

**Na Elizabeth Zaya**

WATANZANIA wameshauriwa kuacha kutumia bidhaa ambazo hazina viwango kwa sababu ya visingizio vya kukwepa gharama.

Akizungumza katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF), Meneja wa Masoko ya Mitandaoni kutoka Kampuni ya Mabati ya Dragon, Elias Frank, alisema bado hakuna elimu ya kutosha kwa idadi kubwa ya Watanzania juu ya matumizi ya bidhaa bora.

"Lipo tatizo la watu kukimbilia kutumia bidhaa zisizo na viwango wakidai wanakwepa gharama kubwa kutumia zile zenye ubora, sasa hili ni tatizo kwa sababu unapotumia bidhaa isiyo na ubora ni lazima itakulazimu ununue mara kwa mara, wakati ukinunua yenye ubora unaweza ukaitumia mpaka miaka yako yote duniani," alisema Frank.

"Mfano mzuri ni kwetu sisi tunaouza bati, tumekuwa tukikumbana na wateja wa namna hiyo, mtu anakuja kwetu anataka bati la bei nafuu, sasa hili ni tatizo badala ya kuangalia ubora anakimbilia kuuliza la bei nafuu. Sisi pia tunapouza bati kwa mtu lazima tumuwekee na warati ya miaka 10 jambo ambalo wale wanaouza zisizo na ubora hawawezi kufanya hivyo, kwa hiyo hata ukimweleza hayo yote haelewi."

## Nyumbu yawapa vijana somo kuhusu teknolojia

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Nyumbu linalojihusisha na uhawilishaji wa teknolojia, limewataka vijana kuacha kuogopa kazi za teknolojia zinazotumia mikono kwa kuwa ni miongoni mwa taaluma muhimu itakayowaletea maendeleo ya kiuchumi.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja Masoko na Mauzo wa Shirika hilo, Mhandisi Robart Chidundo, katika maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba. Chidundo alisema bado lipo tatizo kwa vijana wengi kupendelea kufanya kazi zinazotumia kompyuta pekee, huku wakiziogopa kazi za kiteknolojia.

"Dunia ya sasa bila teknolojia hakuna maendeleo, hatuwezi kukuza uchumi pasipo na teknolojia, kwa sasa shughuli nyingi zinafanyika kwa kutumia zana za kiteknolojia na sisi tumejitahidi kuhakikisha tunatengeneza nyingi ambazo zitasaidia uzalishaji katika sekta mbalimbali, kwenye kilimo, viwandani, ujenzi na maeneo mengine," alisema Chidundo.

Alisema endapo vijana watajiingiza katika sekta hiyo ya teknolojia itawasaidia kupata ujuzi mkubwa na kufungua viwanda vyao na kutengeneza ajira kwa kiwango kikubwa. "Tunataka kwa sasa wabadilike, waone fursa mbalimbali za kiteknolojia na kuzifanyia kazi, waje wajionee na kujifunza kupitia hizi zana mbalimbali zinazotengenezwa na Watanzania wenyewe, tunaamini watabadili mitizamo yao."

Nipashe
Spotika




EURO 2020: TAKWIMU 10 ZA KUVUTIA RAUNDI YA 16 UK. 12 - 13




# RONALDO ANAVYOKIMBIZA KUINGIZA FEDHA INSTAGRAM

**LONDON,** England

CRISTIANO Ronaldo anaongoza orodha ya watu matajiri zaidi duniani kupitia mtandao wa Instagram, kama mtu maarufu anayetoza gharama ya juu kabisa ya matangazo kuliko mtu mwingine yeyote.

Mshambuliaji huyo wa Juventus, anaweza kutoza watu au makampuni yanayotaka kutangaza kupitia ukurasa wake wa mtandao wa Instagram kwa dola milioni 1.6 kwa tangazo moja, hiyo ni kwa mujibu wa Kampuni ya Kimataifa ya Masoko ya Hopper HQ.

Nyota huyo wa zamani wa Klabu ya Real Madrid, amempiku mwigizaji aliyewahi kuwa mwanamieleka, Dwayne "The Rock" Johnson.

Hii ni mara ya kwanza kwa Ronaldo kuongoza kwenye orodha hiyo tangu ianzishwe na kutambulika mwaka 2017.

Mshambuliaji huyo mwenye tuzo tano za Mchezaji Bora wa Dunia 'Ballon d'Or, kwa sasa ana wafuasi milioni 308 kwenye ukurasa wa mtandao wake wa Instagram.

Johnson, ambaye amekuwa akitamba katika filamu za Fast and Furious, ana wafuasi milioni 250, yeye anatoza dola milioni 1.52 kwa tangazo moja, wakati nyota wa muziki wa Pop, Ariana Grande, akiwa nafasi ya tatu akitoza dola milioni 1.51.

Lionel Messi, ambaye wiki hii amekuwa mchezaji huru baada ya mkataba wake na Barcelona kumalizika, yuko kweye kumi bora akishika nafasi ya saba kwa kutoza dola milioni 1.1 kwa tangazo moja. Raia huyo wa Argentina ana wafuasi milioni 224 kwenye ukurasa wake wa mtandao wa Instagram.

Mshambuliaji wa PSG na Brazil, Neymar (dola 824,000) ni miongoni mwa wanamichezo wanaofanya vizuri kwenye matangazo akiwa nafasi ya 16.

Kampuni hiyo ya Hopper HQ yenye makao makuu yake nchini England, inaendesha akaunti za mitandao ya kijamii kwa niaba ya watu ama makampuni, na ilianza kuchapisha orodha hiyo ya watu matajiri kwenye mtandao wa Instagram kuanzia mwaka 2017.

Baadhi ya vigezo inavyotumia kampuni hiyo kuwapata matajiri hao kwenye orodha yake ni pamoja na kuangalia mtu mwenye wafuasi wengi, kwa kiasi gani anachapisha kweye mtandao wake na anavyoshiriki na kushirikishwa na watu wengine kwenye akaunti yake.

Tangu mwaka jana wastani wa gharama ya chapisho moja la tangazo kwa Ronaldo, ambaye aliteka vichwa wiki iliyopita kwa kuondoa chupa za coca-cola kwenye mkutano na wanahabari kabla ya Ureno kukutana na Hungary katika michuano ya Euro 2020, zimeongezeka kwa asilimia 54%.

Wako wanawake sita katika orodha ya matajiri hao 10 wa Instagram ingawa ni kwa mara ya kwanza mwaka huu kwa Kim Kardashian au Jenner hawamo kwenye tatu bora.

"Wakati janga la Covid-19 likiendelea na kuathiri maisha yetu, inaonekana kwamba Instagram ndio mahala pekee ambapo hapajaathirika na janga, watu wameamua kutumia mtandao huu zaidi kuliko wakati mwingine wowote," alisema Mike Bandar, mwanzilishi mwenza wa Kampuni ya Hopper HQ.

"Ni jambo zuri kuona Cristiano Ronaldo akichukua nafasi ya kwanza mwaka huu baada ya kukaa kwenye tano bora kwenye historia ya orodha hiyo.

Orodha kamili ya watu maarufu 10 wanaoweza kutoza gharama kubwa zaidi kwa tangazo kwenye mtandao wa Instagram ni kama ifuatavyo.

**1.** Cristiano Ronaldo, wafuasi milioni 308 - dola mil 1.6 kwa tangazo
**2.** Dwayne "The Rock" Johnson, wafuasi milioni 250 -dola mil 1.52 kwa tangazo
**3.** Ariana Grande, wafuasi milioni 247 - dola mil 1.51 kwa tangazo
**4.** Kylie Jenner, wafuasi milioni 244 - dola mil 1.49 kwa tangazo
**5.** Selena Gomez, wafuasi milioni 241 - dola mil 1.46 kwa tangazo
**6.** Kim Kardashian, wafuasi milioni 232 - dola mil 1.41 kwa tangazo
**7.** Lionel Messi, wafuasi milioni 224 - dola mil 1.16 kwa tangazo
**8.** Beyonce Knowles, wafuasi milioni 189 - dola mil 1.14 kwa tangazo
**9.** Justin Bieber, wafuasi milioni 180 - dola mil 1.11 kwa tangazo
**10.** Kendall Jenner, wafuasi milioni 172 - dola mil 1.05 kwa tangazo.

## ISIKUPITE

TIMU ya Simba haijawahi kupata ushindi ikicheza mbele ya Rais wa Tanzania, mwaka 1993 Kombe la Caf (sasa Kombe la Shirikisho) ilifungwa Uwanja wa Uhuru na Stella Abidjan ya Ivory Coast mbele ya Rais Ali Hassan Mwinyi, ikafungwa na Kagera Sugar na kisha Yanga mechi za Ligi Kuu Bara mbele ya Rais John Magufuli kabla ya juzi kuchapwa na Yanga tena mbele ya Rais Samia Hassan Suluhu.



## Extra Time

# EURO 2020: TAKWIMU 10 ZA KUVUTIA RAUNDI YA 16

**LONDON,** England

UKRAINE ilikamilisha orodha ya timu za robo fainali za Euro 2020 bila kutarajiwa baada ya ushindi dhidi ya Sweden iliyokuwa na wachezaji 10 kwenye muda wa ziada jijini Glasgow. Taifa hilo kutoka Scandinavia lilionekana lisingeweza kufikia hatua ya mikwaju ya penalti baada ya kubakiwa na wachezaji 10 mwanzoni mwa muda wa ziada, lakini Artem Dobvyk alikuwa na mawazo tofauti kabisa.

Mapema siku hiyo, England na Ujerumani walikuwa na mchezo wa kisasi wa kufuzu robo fainali pale katika dimba la Wembley. 'Simba Watatu' hao walipata ushindi baada ya mabao mawili ya kipindi cha pili kutoka kwa Raheem Sterling na Harry Kane. Matokeo hayo yalimaanisha kwamba miamba wote watatu kutoka kundi la kifo, Ufaransa, Ureno na Ujerumani ilitolewa hatua ya 16-bora.

Bingwa mtetezi, Ureno alitupwa nje na Ubelgiji, huku Uswisi wakiwatoa nishai Ufaransa kwa changamoto ya mikwaju ya penalti. Uswisi walifunga mara mbili baada ya kuwa nyuma kwa mabao 3-1 na kulazimisha mchezo kwenda muda wa ziada. Kwenye mchezo wa mepema Croatia nao walitolewa na Hispania katika muda wa ziada.

**Katika makala haya, tunaangalia takwimu za kuvutia kwenye Euro 2020 hatua ya mtoano ya timu 16-bora, twende sasa...**

### #10. UKRAINE KUFUZU KWA MARA YA KWANZA ROBO FAINALI

Hatua ya 16-bora ya michuano ya Euro 2020, hakika ilikuwa ya kuvutia, kwani Ukraine ilionyesha kiwango cha aina yake na kuwafunga Sweden, na kufuzu robo fainali kwa mara ya kwanza kwenye michuano hiyo ya Ulaya. Baada ya Oleksandr Zinchenko kuipa Ukraine uongozi pale Glasgow, Emil Forsberg akasawazisha kwa Sweden na baadaye kulazimika kwenda muda wa ziada.

Cha kufurahisha, Ukraine ilimaliza nafasi ya tatu kwenye kundi lao la kufuzu Euro 2020 na ilitinga kutoka kwenye kapu la washindi bora watatu.

### #9. KADI NYEKUNDU YA KWANZA MUDA WA ZIADA

Licha ya Sweden kugonga mwamba mara mbili na Ukraine mara moja, mchezo huo wa raundi ya 16 ulikwenda muda wa ziada.

Baada ya Sweden kubadilisha mara tatu nafasi ya ushambuliaji kabla ya kwenda kwenye penalti, ujinga wa Marcus Danielson ukawagharimu.

Mlinzi huyo wa kati wa Sweden alikaba vizuri na kupata mpira, lakini akafanya ujinga wa kumkwatua Artem Beseydin. Baada ya marudio ya VAR, mwamuzi hakuwa na namna nyingine zaidi ya kumlima kadi nyekundu ya moja kwa moja.

### #8. ENGLAND KUTORUHUSU BAO MECHI NNE.

England iliweka historia ya kutoruhusu bao kwenye mechi nne za kwanza za mashindano makubwa kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1966 kwenye Kombe la Dunia. Hata hivyo, kwa kuitoa Ukraine juzi kwa ushindi wa mabao 4-0, inafikisha michezo mitano sasa bila kuruhusu bao.

Kabla ya kuanza kwa mashindano haya, England ilikuwa moja ya timu ambayo ilikuwa inapewa nafasi kubwa ya kushinda taji la Euro 2020.

'Simba Watatu' hao waliwafunga Ujerumani 2-0 kwenye Uwanja wa Wembley na kufuzu robo fainali. Matokeo hayo yalimaanisha kwamba, England waliweza kucheza mechi zao za kwanza nne za mashindano makubwa bila kuruhusu nyavu zake kutikiswa kwa mara ya kwanza tangu michuano ya Kombe la Dunia mwaka 196.

### #7. UFARANSA KUTOLEWA MARA TATU BAADA YA MUDA WA ZIADA

Ufaransa ilishindwa kuendeleza moto wake wa kubeba Kombe la Dunia mwaka 2018 baada ya kutolewa na Uswisi kwa changamoto ya mikwaju ya penalti.

Baada ya Uswisi kufunga bao la uongozi na kukosa penalti ambayo ingewafanya kuwa mbele kwa mabao 2-0, Karim Benzema haraka akaifungia mara mbili Ufaransa. Wakati Paul Pogba alipofunga la tatu kwa shuti la mbali, 'Les Bleus' hao wakawa wanaongoza 3-1 zikiwa zimebaki dakika 15 mpira kumalizika ili wafuzu robo fainali.

Lakini mambo yakawa tofauti na Uswisi wakasawazisha mabao mawili na kwenda muda wa ziada, kabla ya penalti ya Kylian Mbappe kuokolewa na Yann Sommer na kuwaondoa mashindanoni Ufaransa.

Hiyo ikawafanya kutolewa kwa mara ya tatu kwenye michunao mikubwa katika muda wa ziada tangu michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2006 walipotupwa nje na Italia. Ufaransa pia ilitolewa na Ureno kwenye muda wa ziada kwenye michuano hiyo mwaka 2016.




Mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe akinyanyuliwa na beki Adrien Rabiot baada ya kukosa penalti dhidi ya Uswisi kwenye mechi ya hatua ya 16-bora Euro 2020. **PICHA: MTANDAO**

### #6. USWISI ROBO FAINALI BAADA YA MIAKA 67

Moja ya vitu vya kuvutia zaidi kwenye michuano ya Euro 2020, ilikuwa ni wakati Uswisi wakiwafunga mabingwa watetezi wa Kombe la Dunia Ufaransa kwa mikwaju ya penalti mjini Bucharest nchini Romania.

Baada ya sare ya mabao 3-3 katika muda wa kawaida na ule wa ziada, Uswisi wakawafunga Ufaransa kwa penalti 5-4 na kufuzu robo fainali ya mashindano makubwa kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 67. Kwa mara ya kwanza walifanya hivyo kwenye Kombe la Dunia mwaka 1954.

### #5. CROATIA VS HISPANIA MABAO MENGI

Mchezo wa Croatia dhidi ya Hispania ndio uliozalisha mabao mengi zaidi wakati wakicheza mjini Copenhagen kwenye Euro 2020 kutafuta nafasi ya kufuzu robo fainali.

Croatia ilianza kuongoza kabla ya Hispania kujibu na mabao matatu na matokeo kusoma 3-1 hadi dakika ya 85. Lakini Mislav Orsic akafunga la pili kwa Croatia kabla ya Mario Pasalic kusawazisha dakika ya 92 na kwenda muda wa ziada. Lakini katika muda wa ziada, Alvaro Morata na Mikel Oyarzabal, kila mmoja akafunga bao moja na kuwatoa Croatia kwenye mashindano hayo.

Idadi hiyo ya mabao nane kwenye mchezo huo, ikafanya kuweka historia ya mabao mengi kwenye mashindano hayo ya Euro 2020.

### #4. PASI NDEFU ZAIDI BAO LA KUJIFUNGA

Wakati Hispania ikitawala mchezo dhidi ya Croaria, Pedri alijaribu kutuliza mashambulizi kwa kurudisha mpira kwa golikipa wake. Pedri alikuwa mbali, karibu na katikati ya uwanja na akaamua kumpasia golikipa wake.

Lakini mpira huo wa pasi ndefu aliyoipiga ulipishana na golikipa wake, Unai Simon ambaye aliuangalia ukiingia langoni mwake bila kufanya lolote. Na hilo likawa bao la kujifunga la pasi ndefu zaidi kwenye mashindano hayo.

### #3. MABAO MENGI YA KUJIFUNGA

Michuano hii ya Euro 2020 hadi hatua ya 16-bora imezalisha mabao mengi zaidi ya kujifunga katika historia yake.

Bao la Perdi la kujifunga kwenye mchezo wa Hispania dhidi ya Croatia, lilikuwa ni la tisa kwenye mashindano ya Euro 2020.

Wachezaji wengine waliojifunga kwenye mashindano hayo kabla ya hatua hiyo ni Merih Demiral, Mats Hummels, Ruben Dias, Raphael Guerreiro, Wojciech Szczęsny, Lukas Hradecky, Martin Dubravka na Juraj Kucka.

### #2. HISPANIA KUFUNGA MABAO MATANO MFULULIZO

Ushindi wa Hispania wa mabao 5-3 dhidi ya Croatia, uliwafanya waingie kwenye vitabu vya kumbukumbu ya mashindano hayo kwa kufunga mabao matano kwenye mechi mbili mfululizo za mashindano ya Ulaya.

Awali, kwenye hatua ya makundi waliifunga Slovakia mabao 5-0.

### #1. ITALIA MECHI 31 BILA KUPOTEZA

Baada ya Italia kushindwa kufuzu kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018 nchini Russia, sasa imeonekana kuwa ya moto chini ya kocha, Roberto Mancini.

'Azzurri' hao wameonyesha kiwango cha kuvutia Euro 2020, ambapo walishinda mechi zao zote tatu za makundi.

Waliifunga Austria kwenye muda wa ziada hatua ya 16-bora na kufikisha idadi ya mechi 31 ambazo hawajapoteza katika mashindano yote hadi sasa. Na hiyo ikaifanya Italia kuivunja rekodi yake ya kucheza mechi 30 bila kupoteza ambayo iliiweka kati ya mwaka 1935 na 1939.

## Nukuu

"TIMU zote zilikuwa na mchezo mzuri na katika mchezo wa leo [juzi], tulitaka kuonyesha jinsi Yanga ilivyokuwa kubwa, kwa upande wangu hii si mara ya kwanza kucheza na Simba, nilikutana nao kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika nikiwa Sudan, pamoja na kupata matokeo haya tusibwete," **Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi baada ya timu yake kuichapa Simba bao 1-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu juzi.**



"Nimewahi kusema kwamba tuzo binafsi ni kitu cha pili - tuko hapa kwa kitu kingine," **Lionel Messi, baada ya kuifungia Argentina bao wakati ikishinda 3-0 dhidi ya Ecuador kwenye michuano ya Copa America juzi.**




"Kazi bado haijaisha. Kuna mpira zaidi wa kucheza, ni nzuri kwa nchi yetu - nusu fainali sasa pale Wembley, kila mtu anaweza kutarajia hilo," **Kocha wa England, Gareth Southgate baada ya kuifunga Ukraine juzi mabao 4-0 na kutinga nusu fainali ya michuano ya Euro 2020.**





Zawadi Mauya (kulia), akishangilia na Deus Kaseke, baada ya kuifungia Yanga bao pekee wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# REKODI ZILIZOWEKWA 'DABI' SIMBA, YANGA

**Na Adam Fungamwango**

ZILIKUWA ni dakika 90 za kukata na shoka za mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara mzunguko wa pili kati ya watani wa jadi, Simba dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikishuhudiwa 'Mnyama' akichinjwa.

Lilikuwa ni bao la kiungo mkabaji, Zawadi Mauya dakika ya 11 akiachia fataki kali lililombabatiza Shomari Kapombe na kujaa wavuni. Mfungaji aliukuta mpira uliokuwa umeokolewa na kipa Aishi Manula kwenye mpira wa kona.

Kwa ushindi huo wa bao 1-0, Yanga inaingia kwenye rekodi nzuri ya kuifunga Simba misimu miwili mfululizo. Msimu uliopita, baada ya sare ya mabao 2-2 Januari 4, mwaka jana, Yanga iliichapa Simba bao 1-0 lililofungwa na Bernard Morrison Mei 8, mwaka jana, ambaye kwa sasa anaichezea wapinzani wao hao.

Msimu huu pia, baada ya sare ya bao 1-1, Novemba 7, mwaka jana, Jumamosi iliyopita Yanga ilishinda bao 1-0.

Kwa misimu yote hii miwili, Simba imekuwa kwenye kiwango bora kabisa, lakini imeshindwa kabisa kupata ushindi kwenye mechi za 'dabi' kwenye Ligi Kuu, kiasi cha kuzua maswali yasiyojibika kwa wanachama na mashabiki wa klabu hiyo.

## KUFUNGWA MBELE YA MARAIS

Kuna rekodi inayojitengeneza kuwa Simba huwa inafungwa pindi Marais wanapokuwa uwanjani.

Acha siku za karibuni, mwaka 1993, Simba ilifungwa kwenye fainali ya Kombe la CAF (kwa sasa Kombe la Shirikisho Afrika) mabao 2-0 na Stella Club Abidjan ya Ivory Coast mbele ya aliyekuwa Rais wa Awali ya Pili, Ali Hassan Mwinyi.

Mei 19, mwaka, 2018, Simba ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu, Simba ikikabidhiwa kombe la ubingwa wa Ligi Kuu, mbele ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Tano, hayati Dk. John Pombe Magufuli.

Simba ilifungwa tena mbele ya Dk. Magufuli kwa mara nyingine tena Mei 8, mwaka jana kwenye mechi ya Ligi Kuu kwa bao 1-0 dhidi ya Yanga.

Juzi tena Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Awamu ya Sita, Samia Suluhu Hassan, aliyekuwa uwanjani hapo, ilishuhudiwa kwa mara nyingine Simba ikipoteza kwa bao 1-0 mbele ya Yanga.

## MAKOCHA WA AL MERRIKH

Kwenye mechi hiyo ya 'dabi', timu zote zilikuwa na makocha wapya tofauti ya wale wa mzunguko wa kwanza msimu huu, wote wakiwa wameifundisha Al Merrikh ya Sudan.

Simba ilikuwa na Didier Gomes da Rosa aliyejiunga na timu hiyo Januari mwaka huu baada ya kuvunja mkataba na timu hiyo maarufu nchini Sudan, huku Kocha Mkuu wa Yanga, Mtunisia Nasreddine Nabi akijiunga na Yanga katikati ya Aprili.

Kocha Nabi alijiunga na timu hiyo ya Sudan, baada ya Gomes kuondoka, ingawa hakudumu kwa muda mrefu, akatimuliwa baada ya kutoka suluhu na Simba kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza zilipotoka sare ya bao 1-1, Simba ilikuwa na Mbelgiji Sven Vandenbroeck, Yanga ikiwa na Mrundi, Cedric Kaze.

## MANULA, MAUYA WAWEKA REKODI

Wakati Zawadi Mauya akiweka rekodi ya kufunga mechi yake ya kwanza ya 'dabi', akiwa amesajiliwa msimu huu akitokea Kagera Sugar, Aishi Manula ameweka rekodi ya kucheza 'dabi' zote tangu ajiunge na timu hiyo 2017/18 akitokea Azam FC.

Manula ndiye amekaa golini mechi zote za Simba ikicheza na Yanga kwa misimu minne sasa.

## YANGA YAZIDI KUITESA SIMBA

Kwa ushindi wa Jumamosi, Yanga imezidi kuongeza wigo wa kuifunga Simba mara nyingi zaidi kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara tangu mwaka 1965.

Tayari timu hizo zimekutana mara 106, Yanga sasa imefikisha mechi 38 za kuifunga Simba, huku Wekundu wa Msimbazi, wakiwa wamepata ushindi mara 31 tu, timu hizo zikitoka sare mara 37.

Yanga imefikisha mabao 151 ya kufunga kwenye mechi za 'dabi', huku Simba ikiwa imefunga mabao 136.

Wanajangwani hao wameweka rekodi nyingine ya kutoka uwanjani bila kuruhusu bao kwenye mechi za watani mara 44 sasa, huku Simba ikiwa ina rekodi kama hiyo mara 32 tu, kwa mechi zao 106 walizocheza mpaka sasa.

## JE, WAJUA?



SERGIO Ramos ndiye beki anayeongoza duniani katika karne hii ya 21 kwa kufunga mabao mengi zaidi (mabao 104), akifuatiwa na John Terry (67) na Naldo (65).





## Chamwino waaswa maambukizi ya VVU

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

WAKAZI wa Wilaya ya Chamwino, wametakiwa kuacha mila na desturi potofu ya kufanya mikesha usiku, ambayo imekuwa ikichangia kwa kasi maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Tarafa ya Chamwino, Mohamed Mfaki, alipokuwa akizungumza na viongozi mbalimbali wa serikali na dini ngazi ya kata na vijiji wa Kata ya Buigiri, kwenye semina juu ya kutambua mila na desturi potofu zinavyosababisha maambukizi ya Ukimwi.

Mfaki akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya hiyo, alisema mikusanyiko ya mikesha inayofanyika imekuwa ni sehemu moja ambayo inasababisha maambukizi ya VVU.

Alisema mikesha hiyo ambayo imekuwa ikifanyika usiku, inachangia kuenea maambukizi ya magonjwa mbalimbali yakiwamo VVU, hivyo jamii inatakiwa kujiepusha kwa kuwa haina tija zaidi ya kupoteza nguvukazi.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chamwino, Keneth Yindi, alisema wakati umefika kwa wananchi kuwa na elimu ambayo itakayowasaidia kuacha mila na desturi potofu.

Naye Mchungaji Samson Damasi, wa Kanisa la Angalika Chinagali wilayani Chamwino, alisema mila na desturi ya kurithiana wajane na wagane pamoja na ndoa za utotoni zimekuwa chanzo kikubwa cha maambukizi ya VVU.

Mchungaji huyo, alisema pia mila za ukeketaji na tohara zimekuwa zikichangia kuwapo kwa ongezeko la maambukizi, kutokana na kutumika kwa kifaa kimoja.

# Mkumbo aja na mkakati sera zilizopitwa na wakati

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amesema wanapanga kuzipitia sera zote zilizopitwa na wakati ili ziendane na wakati uliopo.

Prof. Mkumbo aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na watumishi wa wizara hiyo kwa mara ya kwanza tangu ateuliwe katika nafasi hiyo na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema wizara yake inapanga kufanya hivyo ili kuweka mazingira rafiki ya ufanyaji biashara.

"Nimewaelekeza wenzangu lazima tuhuwishe sera zote katika Wizara ya Viwanda na Biashara zilizopitwa na wakati na iwe mwisho kuishi na sera zilizopitwa na wakati," alisisitiza Prof. Mkumbo.

Alisema kuwa jukumu la kwanza la kila wizara ni sera na siyo kuendelea kukaa na zile ambazo zimepitwa na wakati.

"Tusifanye majukumu ya wenzetu tufanye kazi zinazotuhusu sisi kama wizara nataka yale yaliyondani ya uwezo wangu tuyafanyie kazi," alisema.

Kadhalika, alisema ni lazima wizara izifanyie marekebisho sera pamoja na sheria ili kubaini zenye changamoto na kuzifanyia kazi.

Aidha, alisema ni lazima watumishi wa wizara hiyo kuwa wa kwanza kubaini mapungufu yaliyopo katika sera na sheria na siyo kuwaachia wafanyabiashara.

"Lazima hili mlifanye nyie katika idara yenu ya sheria kutambua changamoto zilizopo katika sera na sheria zetu ili kuzifanyia marekebisho kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika sekta ya viwanda na biashara," alisema.

Vilevile, aliwataka watumishi wa wizara hiyo kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sera, sheria na taratibu na wanapoona kuwa kuna upungufu hawanabudi kumshauri waziri.

Alisema kuwa ameteuliwa kuongoza wizara hiyo na Rais, hivyo ni wajibu wake kutimiza matarajio ya Watanzania katika sekta ya viwanda na biashara na siyo vinginevyo.

"Mimi napenda sana kukosolewa na siyo kusifiwa, naomba watumishi nyie ndiyo wataalamu ...msiwe kama sisi wanasiasa, nataka unaponishauri nishauri kwa mujibu wa sera na sheria na siyo busara zako hizo," alisema.

Pia alisema kutokana na wizara hiyo kuwa kati ya kongwe, wamepanga ifikapo 2025 pato la Mtanzania linakua kutoka Dola za Marekeni 1,080 za sasa hadi 3,000.

Prof. Mkumbo alisema hivi sasa moja katika kero inayovikabili viwanda ni uhaba wa malighafi kwa ajili ya uzalishaji bidhaa.

"Viwanda vyetu vinafanya kazi chini ya kiwango kwa sababu hatuna malighafi za kutosha, viwanda vyetu vingine vimefungwa na vingine vinazalisha kwa muda mfupi tuu," alisisitiza Prof. Mkumbo.



Mkulima wa zabibu Kijiji cha Hombolo mkoani Dodoma, Evarist Maganga (kulia), akitoa maelezo ya kilimo cha zao hilo kwa Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA), mkoani humo, Idd Senge na Kemi Kalikawe, walipotembelea wakulima hao mwishoni mwa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kasi migogoro ya ardhi yamkera Mtaka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amesema kwa kipindi cha siku 30 alichokaa katika ofisi yake mpya amekuwa akipokea wananchi kati ya 100 hadi 130 kwa siku wenye malalamiko ya ardhi.

Mtaka, aliyasema hayo kwenye kikao cha kujadili kero ya ardhi katika Jiji la Dodoma, kilicho wahusisha viongozi wa Chama Cha Mapinduzi, viongozi wa mabaraza ya ardhi pamoja na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Alisema Dodoma pamoja na kuwa makao makuu, lakini bado kuna kero kubwa ya migogoro ya ardhi, ambayo inatakiwa kutatuliwa.

"Tangu nimeingia ofisini kwa muda wa siku 30, ofisini kwangu nimekuwa nikipokea wananchi wenye malalamiko ya ardhi kati ya 100 hadi 130 kwa siku, jambo ambalo ni tatizo kubwa.

"Nimeona kuwa haiwezi kuwa jambo jema Jiji la Dodoma kuwa sehemu ya migogoro kwani kuwapo migogoro ya ardhi isiyoisha, hatuwezi kuwa na maendeleo," alisema Mtaka.

Pia alisema kutokana na hali hiyo, ameona ni vyema kuitisha kikao ili kujadili jambo hilo na kulitafutia ufumbuzi.

Alisema wamepanga kutumia ukumbi wa Jakaya Kikwete kusikiliza kero za ardhi kwa siku tatu kwa watu wenye migogoro wakiwa na nyaraka zao.

"Lakini tutatumia siku saba kwa ajili ya kutembelea kata zote 41, ili kubaini ni kata ipi inaongoza kwa kuwa na migogoro, kwa lengo la kuhakikisha tunakuwa na Dodoma Jiji isiyokuwa na migogoro," alisema Mtaka.

Katika hatua nyingine, Mtaka alisema baada ya kumaliza migogoro katika Jiji la Dodoma wataanza kutembelea wilaya zote kubaini ni wapi kuna migogoro na jinsi ya kuitatua.

"Nia ni kuona Dodoma ambapo wanaishi viongozi, Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na viongozi wengine panakuwa sehemu ambayo haina migogoro na kuwapo na utulivu," alisema.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, aliwaagiza kwa wakuu wote wa mikoa na wilaya kuwa na madaftari yanayobainisha kiwango cha migogoro ya ardhi katika maeneo yao.

Aidha, Lukuvi alisema ni marufuku kwa watendaji wote wa mitaa iliyopo mijini kuuza maeneo.



# Wadau walalamikia trafiki chanzo cha ajali barabarani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa usafirishaji mkoani Mbeya, wamewalalamikia maaskari wa Kikosi cha Usalama Barabarani kwa madai ya kusababisha ajali za barabarani kutokana na tabia zao ikiwamo lugha za vitisho kwa madereva na kusimamisha magari ghafla.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini na wadau wa usafirishaji wakati wa kikao maalumu kilichoitishwa na Jeshi la Polisi ili kujadili na kuweka mikakati mbalimbali ya kumaliza ajali za barabarani mkoani humo.

Kikao hicho kiliwashirikisha wakaguzi wa magari kutoka Jeshi la Polisi, wamiliki wa mabasi ya masafa marefu na mafupi, madereva, maofisa usafirishaji (wapiga debe) na mabalozi wa Usalama Barabarani mkoa wa Mbeya.

Mmoja wa wadau hao, Peter Salim, ambaye ni wakala wa moja ya kampuni za usafirishaji, alisema baadhi ya maaskari wa usalama barabarani wanatumia lugha za vitisho kwa madereva hali inayowatia hofu madereva hao.

"Askari anasimamisha gari halafu anaanza kulikagua kisha anamwambia mwenzake aandike faini huku akidai kuwa gari ni bovu huyu dereva lazima nimpeleke mahakamani nimfunge, sasa dereva siku nzima anakuwa anaendesha gari huku akiwaza kufungwa, anaweza akafika muda akaangusha gari," alisema Salum.

Naye Sara Mwambapa, ambaye ni matroni wa stendi kuu ya Mbeya, alisema baadhi ya maaskari huwa wanasimamisha magari ghafla hali ambayo wakati mwingine gari likiwa na mwendo mkali inaweza kusababisha ajali.

Alisema baadhi ya maaskari hao hujificha vichakani na kupiga tochi magari yanayoenda kwa mwendo kasi jambo ambalo alidai ni kinyume na utaratibu wa kudhibiti mwendokasi.

"Lakini mabasi yote ya masafa marefu yamefungwa ving'amuzi ambavyo ndivyo vinavyodhibiti mwendo wa mabasi, sasa kwanini hizi tochi zisiondolewe barabarani ili vibaki ving'amuzi ambavyo ndio teknolojia ya kisasa?" Alihoji Sara.

Mabalozi wa usalama barabarani Mkoa wa Mbeya walisema ili kuboresha sekta ya usafirishaji katika mkoa huo, wameandaa mafunzo maalumu ya usafirishaji unaozingatia sheria kwa wapigadebe wote wa mkoa huo ambayo alisema yatafanyika hivi karibuni.

Frorencia Bisa, ambaye ni Mwenyekiti wa mabalozi hao, alisema mafunzo hayo yatawahusu wapigadebe wote na baada ya mafunzo hayo, washiriki wote watapatiwa vyeti maalumu vya kuwatambua na wale ambao hawatahudhuria wataondolewa kwenye kazi hiyo.

"Maaskari wakimkuta mtu ambaye hajapata mafunzo hayo halafu anafanya kazi, watamkamata na kumshughulikia kama mhalifu mwingine, tutaweka utaratibu mzuri ambao kila mmoja atashiriki," alisema Florencia.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema aliamua kuitisha kikao hicho ili kupata suluhu ya ajali ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu.

Alisema wataendelea kuitisha vikao vya aina hiyo na makundi mbalimbali ili kuhakikisha wadau wote wa usafirishaji wanashiriki kwenye vita ya kukomesha ajali mkoani humo.

Alisema pamoja na vikao hivyo pia jeshi hilo litaendelea kufanya ukaguzi wa mabasi yote yanayosafirisha abiria mkoani humo ili kuhakikisha yanaondoka yakiwa imara.



Ofisa Mtendaji wa Kata ya Miyombweni wilayani Mbarali, Anganile Luvanda, akiwasilisha taarifa ya mradi wa ujenzi wa vyoo na kisima cha maji katika Zahanati ya Kijiji cha Mlungu, mwishoni mwa wiki. Mradi huo umetekelezwa na Shirila la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) chini ya mradi wa SAWA. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watendaji wapewa pikipiki 20 kuboresha huduma

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Maji Mkoa wa Mbeya (Mbeya-WSSA), imegawa pikipiki 20 kwa watendaji wake ili kuboresha utendaji kazi wao hasa kuwafikia wananchi na kuboresha huduma za maji kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Edna Mwaigomole, alikabidhi pikipiki kwa watendaji hao mwishoni mwa wiki wakati wa hafla maalumu iliyofanyika katika Ofisi za Mamlaka hiyo zilizopo jijini Mbeya na kuwataka kuzitunza.

Aliwataka wazitumie kwenye shughuli za kuwahudumia wananchi kwa kufika kwa wakati kutatua matatizo ya maji pale wanapopata taarifa za kukosekana kwa huduma hiyo.

"Bodi inawapongeza watu wa menejimenti kwa kutambua mchango wa watendaji hawa na kuamua kuwanunulia vitendea kazi hivi, tunaamini kwamba pikipiki hizi zitasaidia kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wananchi wetu," alisema Mwaigomole.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa mapema linapotokea tatizo lolote la maji kwenye makazi yao ili maofisa hao wawafikie haraka na kurekebisha ili waendelee kupata huduma.

Mkurugenzi wa Mbeya-WSSA, Gilbert Kayange, alisema waliamua kununua pikipiki hizo ili kuongeza ufanisi wa kuwahudumia wananchi na kwamba watendaji hao wamegawanywa katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

Alisema kila mmoja ana eneo lake la kuwahudumia wananchi na akawataka watendaji hao kila mmoja kutimiza wajibu wake ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa ufanisi.

"Huu utaratibu ni sehemu tu ya mikakati yetu, lakini ipo mikakati mingine ikiwamo kubuni vyanzo vipya vya maji, kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa kutumia njia za kielektroniki na kuanza kutumia mita za lipa kabla (Mita za Luku)," alisema Kayange.

# Wananchi waridhia mpango matumizi bora ardhi

**Na Nebart Msokwa,** MAKETE

WANANCHI wa vijiji vitatu vya Wilaya ya Makete mkoani Njombe, wameridhia mpango wa matumizi bora ya ardhi kufanyika katika vijiji vyao ili kuepuka migogoro inayoweza kutokea baina ya wakulima na wafugaji na kutunza vyanzo vya maji.

Mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji hivyo ambavyo ni Isapulano, Ivirikinge na Mwakavuta umefadhiliwa kwa ushirikiano kati ya Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi na Mradi wa Panda Miti kibiashara.

Ofisa Ardhi wa Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi, Emmanuel Mabula, alisema taasisi hiyo ambayo ni chombo cha serikali inawashirikisha wananchi pamoja na wataalamu mbalimbali wa kila kijiji ambacho kinaandaliwa na mpango huo.

Alisema baada ya wananchi kuridhia wanaandaa ramani ya kijiji na picha za anga kwa ajili ya kwenda kuandaa mpango huo na kisha kuwarejeshea tena wananchi kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

"Huu mpango pia utawasaidia wananchi hawa kuepuka uchomaji moto ambao huwa unaathiri miti waliyopanda, tunawashirikisha kwa sababu wao ndio wenye matumizi na ardhi hii," alisema Mabula.

Alisema katika mpango huo yanaandaliwa maeneo kwa ajili ya kilimo, makazi, kuchungia, vyanzo vya maji na shughuli zingine za kijamii ikiwamo maeneo ya kuzika ili kuepusha shughuli hizo kuingiliana.

Mwakilishi wa Mradi wa Panda Miti Kibiashara, Andrew Ferdinand, alisema mpango huo utasaidia kutunza mazingira katika vijiji hivyo kwa maelezo kuwa wananchi hao watakuwa na uwezo wa kuilinda misitu na vyanzo vya maji visiharibiwe.

Vilevile, alisema mpango huo utasaidia kupunguza umaskini katika vijiji hivyo ambavyo vitatekeleza mpango huo kwa maelezo kuwa watafanya shughuli nyingi za kimaendeleo wakishirikiana na wadau mbalimbali.

"Sisi tutashirikiana na vijiji hivi kwenye shughuli muhimu, tutaendelea kutoa elimu ya upandaji miti kibiashara ili wakabiliane na umaskini kupitia raslimali hizo muhimu, lakini watatunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi," alisema Ferdinand.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Isaplano, walisema mpango huo utawasaidia kupunguza migogoro ya ardhi kutokana na wote kushirikishwa kuanzia hatua ya awali mpaka ya mwisho.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Isapulano, Mwatindi Mbilinyi, alisema kuna baadhi ya maeneo wametenga kwa ajili ya kupanda miti ya mbao na baadhi ya kutunza vyanzo vya maji ili kukabili matatizo ya kimazingira.

"Huu mpango una faida kubwa sana, sisi tumeuridhia na tunaamini utatusaidia kutokana na shughuli zetu ambazo ni kilimo na ufugaji shughuli hizi kwa mujibu wa mpango huu hazitakuwa zinaingiliana," alisema Mbilinyi.

Nao viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete walisema, wataendelea kuhamasisha vijiji vingine vya wilaya hiyo ili navyo viingie kwenye mpango huo kwa kuwa una faida kimaendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Francis Namaumbo, alisema mpango huo utakuwa na manufaa kwa halmashauri ya wilaya hiyo na mwananchi mmoja mmoja.



# Mfumuko wa bei wapanda kwa 1.9 %

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MFUMUKO wa bei wa bidhaa kwa mwezi wa Juni 2021 Zanzibar umepanda na kufikia asilimia 1.9 ikilinganishwa na mwezi wa Mei ambao ulikuwa 0.8.

Hayo yalielezwa jana na Mkuu wa Kitengo cha Faharisi za bei kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Khamis Abrahman Mshamu, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mazizini nje ya Mji wa Zanzibar kuhusu mfumuko wa bei wa bidhaa.

Alisema mfumuko wa bei wa chakula na vinywaji visivyokuwa na vileo umeshuka na kufikia asilimia 0.1 ikilinganishwa na asilimia 0.4 mwezi Mei.

Alisema mfumuko wa bei wa chakula umefikia asilimia 0.2 ikilinganishwa na asilimia 0.4 kwa mwezi wa Mei na fahari za bei kwa mwezi wa Juni 2021 zilikuwa 117.7 na Juni 2020 ni asilimia 117.5.

Alisema mfumuko wa bei usio wa chakula umeongezeka kufikia asilimia 3.2 kwa Juni na Mei ulikuwa 0.1 na kuongezeka kwa mfumuko huo kumesababisha kuongezeka kwa bei za bidhaa.

Alizitaja bidhaa hizo kuwa ni mchele wa Thailand asilimia 7.0, unga wa ngano 9.6, samaki 7.7, mafuta ya taa 33.0, petroli 42.2 na dizeli 28.7.

Aidha, alisema mfumuko wa bei wa mwezi kwa fahari ya Juni mwaka 2021 umefikia asilimia 0.3 ikilinganishwa na asilimia 1.1 ya mwezi wa Mei na mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula na vinywaji visivyo na vileo umefikia asilimia 1.7 ikilinganishwa na 2.2 mwezi wa Mei.

Alisema kushuka kwa mfumuko wa bei wa mwezi kumesababisha kushuka kwa bidhaa kama unga wa ngano kwa asilimia 0.7, samaki 0.2, ndizi za mtwike 11.8 na sukari 1.1.

Naye Mhadhir wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Estella Ngoma, alisema sababu za mfumuko wa bei ni kupanda kwa bidhaa ikiwamo mafuta ya petroli na dizeli na kusababisha bidhaa nyingine kupanda bei.

Kwa upande wake Meneja wa Uchumi kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Ofisi ya Zanzibar, Moto Lugobi, alisema, corona imeathiri mfumuko wa bei kwa namna mbili na usafirishaji wa chakula kwa Tanzania haukuathirika sana.

Pia alisema athari nyingine ya corona ni kushuka kwa bei za mafuta na uzalishaji wa viwanda kwa baadhi ya nchi huku Tanzania ikiwa ya moja ya nchi zilizoathirika.

Alisema kwa upande mwingine corona imeathiri uchumi wa nchi kwa ujumla ikiwamo katika sekta ya utalii ambayo ni kubwa inayoendesha uchumi wa Zanzibar.

## Wanafunzi wahamasishwa kupata mwongozo kujiunga elimu ya juu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Makamu wa kwanza wa Rais, Zuhra Kassim Ali, amewataka wazazi, walezi na wanafunzi wanaotaka kujiunga katika elimu ya juu kutembelea katika maonyesho ya vyuo vikuu ili kujua miongozo ya taratibu za kujiunga na taasisi ya vyuo vikuu nchini.

Akizungumza wakati alipotembelea maonyesho ya pili ya elimu ya juu Zanzibar yanayoendelea katika viwanja vya Mapinduzi Square Michenzani mjini hapa, alisema kujitokeza kwao kutasaidia kujua jinsi ya kujiunga na elimu za juu na kutambua fursa za kimasomo zinazopatikana ili kujiendeleza kielimu.

Zuhura, alisema kuwapo kwa maonyesho hayo ni fursa pekee ya kupata uelewa jinsi ya kujiunga katika taasisi mbalimbali za kielimu kwa masomo ya elimu ya juu ni kujitokeza katika maonyesho hayo na kupata mwongozo kutoka kwa wahusika.

Pia alisema hatua hiyo itasaidia kutoa miongozo na ushauri wa kielimu ya kujiunga na masomo kwa mujibu wa viwango vyao vya ufaulu pamoja na kutambua fursa za mikopo ya kimasomo ndani na nje ya nchi.

"Watu ni wachache inawezekana labda hawana taarifa hivyo ni vyema wanafunzi na wazazi wangejitolea kwa sababu taasisi za elimu zimekuwa zikitoa huduma mbalimbali ambazo ni muhimu kwa wanafunzi," alisema.

Kwa upande wao washiriki wa maonyesho hayo wameipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuandaa maonyesho hayo ambayo yanawawezesha kujitangaza kupitia huduma zao wanazotoa.

Mshiriki wa maonyesho hayo, kutoka Taasisi ya Cari vision Study Universities iliyopo Zanzibar ambayo inashughulikia na masuala ya kielimu, Yusuph Seleman, alisema katika taasisi yao wamekuwa wakishiriki kuwapatia ushauri wanafunzi mbalimbali jinsi gani ya kujiandaa kujiunga na elimu ya juu.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akipata maelezo kutoka kwa wajasiriamali walioshiriki katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Ushirika Duniani, yaliyofanyika katika ukumbi wa Shekhe Idriss Abdulwakili. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali kuendelea kuthamini vyama vya ushirika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema serikali yake itaendelea kuthamini mchango mzuri unaotolewa na vyama vya ushirika katika kuimarisha hali za maisha ya wananchi kiuchumi na kijamii.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman, alieleza hayo katika hotuba aliyoisoma kwa niaba ya Rais Dk. Mwinyi katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Ushirika Duniani iliofanyika jijini hapa.

Alisema, serikali imedhamiria kuingia katika uchumi wa bluu kwa lengo la kutumia rasilimali za bahari ili kuleta mapinduzi ya kiuchumi na vyama vya ushirika vina jukumu kubwa la kushirikisha makundi yote yaliyomo katika jamii ili kufikia lengo hilo lililokusudiwa.

Makamu wa Pili wa Rais alisema jamii ina paswa kufahamu kwamba mbali na maeneo makuu ya uchumi wa bluu ambayo ni machimbo ya mafuta na gesi, ujenzi wa viwanda vya uvuvi, usafirishaji na utalii, dhana ambayo imepanga kushirikisha makundi yote katika jamii ikiwamo makundi ya vijana, watu wenye mahitaji maalum, wanawake na wazee.

Alisema, vyama vya ushirika vina wajibu wa kuendeleza uzalishaji wa mazao ya ardhini yakiwamo, mboga, matunda, maziwa, nafaka, mazao ya mizizi na mingineyo ili kuwalisha wananchi na wawekezaji watakao kuja kuwekeza katika shughuli za uchumi wa bluu.

"Ustawi wa vyama hivi haujafikia kiwango vya kuridhisha vikilinganishwa na vyama vya wenzetu nchi jirani, tunataka kuona vyama vipo imara, kimuundo na uendeshaji," alisema Dk. Mwinyi katika hotuba yake. Dk. Mwinyi alisema Zanzibar imedhamiria kuimarisha matumizi ya teknolojia za habari katika uendeshaji wa shughuli za kiuchumi na vyama hivyo vitasaidia kuleta msukumo wa jamii kutumia teknolojia hizo.

Alisema, matumizi hayo ya teknolojia yatasaidia kwa kiasi kikubwa kutoa faida nyingi za kiuchumi zinazopatikana ikiwamo ununuzi wa mazao ya jumla, kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa bidhaa shindani kwenye soko la ndani masoko ya kikanda (SADE na COMESA), hadi kufikia masoko ya kimataifa.

Akizungumzia faida zitokanazo na ushirika, Makamu wa Pili wa Rais, alisema vyama vya ushirika ni taasisi muhimu za hiari zenye uwezo wa kutatua changamoto za kimaisha, kiuchumii na kijamii kwa wananchi wake na kuleta ustawi wa maisha yenye neema kwa jamii.

"Hivi sasa vyama hivi vinatoa fursa kwa wanachama wake kujiajiri na kuajiri wengine, vina uwezo mkubwa wa kuongeza uzalishaji mali na bidhaa mbalimbali," alisema.

Aliutaka uongozi wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais kuwajengea uwezo, kuvikagua na kuvisimamia vyama vya ushirika kwa lengo la kutoa haki na kuondoa manung'uniko ya wanachama.

Alisema, wakati umefika sasa wa kuviunganisha vyama vya ushirika Zanzibar katika ushirikiano wa kimataifa unaohusiana na masuala ya ushirika kutokana na fursa nyingi za kielimu sambamba na kubadilishana uzoefu, matumizi ya teknolojia, mbinu za usimamizi, ubunifu na mtandao wa masoko.

"Katika hatua za kuimarisha vyama ushirika inatulazimu kuhimiza matumizi ya Teknolojia ya Habari (TEHAMA), katika uendeshaji wao, kufanya hivyo itasaidia kupata taarifa sahihi na za uhakika kujifunza kutoka kwa wengine na kudhibiti mapato ya wanachama," alisema.

Akisoma risala kwa niaba ya wanaushirika Katibu wa Muungano wa Vyama vya Ushirika (CUZA), Suleiman Mbarouk Ame, alisema umoja wa wanaushirika utaendeleza jitihada kupitia sekta mbalimbali ikiwamo kushiriki katika masuala ya kilimo cha baharini na nchi kavu.

Suleiman alisema miongoni mwa mafanikio walioyapata vyama vya SACCOS vimefanya kazi kubwa ya kujenga mtaji unaofikia Sh. bilioni 18.2 hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu kupitia michango ya kuweka akiba na amana za wanachama kupitia SACCOS 216 za Unguja na Pemba, fedha ambazo zinatatua changamoto za mtaji kwa wanachama wake.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhani Soraga, alisema vyama vya ushirika ni taasisi muhimu za kiuchumi na zaidi ya asilimia 20 ya nguvu kazi imejiajiri au kuajiriwa kupitia sekta ya vyama vya ushirika.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI YA KAZI

**Nafasi za Kazi ya ualimu diploma science na hesabu 0783298900**

**Kwa Habari Motomoto**

**usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**NDUGU IBRAHIM SUED LEMA** anatangaza kupotelewa na hati ya Nyumba yenye **TITLE DEED PLOT NO 59 BLOCK C** Eneo la **OYSTERBAY HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya polisi namba **DOD/DOD/RB/49113/2021**

116343902

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TARIME**

**RUFAA NA. 156 YA 2071**

**MUHERE MWITA MARWA....................................................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**WAMBURA WARYUBA NYANGIR.........MRUFANIWA**

Mrufaniwa WAMBURA WARYUBA NYANGIRA popote ulipo. Fahamu kwamba mrufani MUHERE MWITA MARWA ameleta rufaa Na.156/20179, dhidi yako. Hivyo basi kama unakusudia kupinga rufaa hiyo unatakiwa kuleta majibu yako na uwepo barazani wewe binafsi, wakili wako au mwakilishi anayekubalika kisheria, tarehe 31/08/2021, siku ambayo shauri limepangwa kutajwa. Endapo hutatekeleza hayo, shauri litaendelea upande mmoja dhidi yako na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 1/06/2021.

NGUKULIKE, N.O

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) TARIME.

116343802

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.........2021**

**In the matter of the Estate of the late DORIS MANYIKA PALLA of IPAGALA Area within Dodoma Region.**

**And**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ANGEROUS ALPHONCE PALLA**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS claiming** to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 23rd day of JULY 2021.

**Dated at Dodoma this 16th day of JUNE 2021.**

RESIDENT MAGISTRATE

116343102

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi NO.179/2021**

**Ombi la MSAFIRI JUMA KIWAMBO Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu JUMA ISMAIL KIWAMBO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 08/07/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 08/06/2021

116343302

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# MOI yaleta matumaini wanaopatwa kiharusi

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Mifupa (MOI) imeanzisha utoaji wa huduma ya kuleta nafuu kwa haraka kwa wagonjwa wanaopata kiharusi na kuwahishwa kwenye huduma katika taasisi hiyo ndani ya saa sita hadi 12.

Akizunguma katika banda la taasisi hiyo kwenye Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF), Muuguzi katika chumba cha upasuaji kutoka taasisi hiyo, Juma Rehani, alisema ndani ya saa hizo sita hadi 12 mgonjwa wa aina hiyo akiwahishwa kufanyiwa uchunguzi na kutibiwa katika taasisi hiyo anaweza kupata nafuu na kurudi katika hali yake ya kawaida.

"Na siyo tu kwenye ubongo, pia kwenye uti wa mgongo na sehemu mbalimbali za mwili. Wagonjwa waliopata kiharusi, ndani ya saa sita mpaka 12 wakifika kwenye huduma hii anaweza akapata nafuu na akarudi kwenye hali yake ya kawaida," alisema Rehani.

Alisema huduma hiyo ya tiba ni mpya na imeanza tangu Januari mwaka huu na hutolewa bila kupasua kwenye eneo la mwili ambalo linakuwa limeganda damu badala yake hutumia tundu dogo kupitia sehemu ya nyonga kuingiza mpira.

Alisema huduma hiyo inahusika zaidi na wagonjwa ambao wamepata matatizo ya kwenye mishipa ya damu iliyopo kwenye ubongo.

"Katika ubongo kuna mzunguko wa mishipa ya damu ambayo ikitokea ikipata hitilafu na damu ikaganda, na inapoganda kwa kutumia upasuaji wa kawaida, huwezi kutoa tone la damu lililoganda, kwa hiyo njia ya kisasa ambayo inatumika ni kutumia mipira kupitia kwenye nyonga kupitia mshipa mkubwa ambao unapeleka mpaka kwenye ubongo," alisema Rehani.

"Kuna wale wagonjwa ambao wanakuwa wamepata kitu kinaitwa kiharusi ambao damu imevujilia kwenye ubongo ambao katika kupitia mashine ya kisasa ambayo kwa Afrika Mashariki na Afrika ya Kati inapatikana MOI peke yake, ina uwezo mkubwa sana wa kufanya uchunguzi pamoja na matibabu kwenye mishipa ya damu."

Alisema tangu huduma hiyo ianze, tayari wameshawahudumia wagonjwa 27, na kwamba bado wanaendelea kutoa elimu kwa jamii ili wale waliokuwa wakipewa rufani kwenda kutibiwa hospitali nje ya nchi watibiwe katika taasisi hiyo.

"Na tunaendelea na taratibu za kutoa matibabu, kufanya uchunguzi, hivyo mtu akipata matatizo akifika MOI atakutana na madaktari bingwa watamwangalia na baada ya hapo watampeleka kwenye uchunguzi kujua tatizo la mshipa wa damu limetokea sehemu gani ya ubongo au sehemu gani ya uti wa mgongo," alisema Rehani.

"Lakini kuna wale ambao wanakuwa wamepata uvimbe kwenye ubongo na wanahitajika kwenda kufanyiwa upasuaji wa kufungua fuvu, kwa kutumia mashine hii ina uwezo wa kutumia mpira kwenye kitundu kidogo na kwenda kufunga ile mishipa ya damu ambayo inaenda kwenye ule uvimbe ili kupunguza uwezekano wa mgonjwa wakati wa kufanyiwa upasuaji asivuje damu kwa wingi."

"Kwa hiyo tunapofunga mishipa ya damu inarahisisha upasuaji kwa njia ya usalama zaidi."



Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo (katikati), akiangalia vipeperushi mbalimbali kuhusu huduma zinazotolewa na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba), jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

## NIT: Tutakuwa nembo ya urafiki China, Tanzania

**Na Prosper Makene**

MKUU wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa, amesema kukamilika kwa chuo chao kuwa Chuo Kikuu cha Usafirishaji kutafanya NIT kuwa na nembo kuu mpya ya urafiki kati ya serikali ya watu wa Jamhuri ya China na Tanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari katika kampasi kuu ya chuo hicho Mabibo jijini Dar es Salaam, Prof. Mganilwa alisema mipango ya kuanza kwa ujenzi wa chuo kikuu hicho upo katika hatua nzuri za utekelezaji.

"Kutokana na urafiki wa muda mrefu tulionao kati yetu na serikali ya watu wa China, ni imani yangu kuwa upanuzi wa chuo hiki kuwa Chuo Kikuu utaifanya NIT kuwa nembo mpya ya urafiki kati ya China na Tanzania," alisema Mkuu wa Chuo.

Aliongezea: "TAZARA ndiyo iliyokuwa nembo kuu ya urafiki kati ya Serikali ya China na Tanzania, lakini hivi sasa shirika hilo halifanyi vyema, hivyo kukamilika kwa mradi huu wa kukigeuza chuo chetu kuwa chuo kikuu utakuwa ndiyo nembo kuu ya urafiki wetu."

Aliongeza: "Tunaishukuru sana Serikali ya China kwa msaada wao, tupo katika hatua nzuri ambapo hivi sasa tunasubiri watie saini maamuzi ya mwisho ili kuruhusu mradi kuendelea na hatua nyingine ya utekelezaji wa ujenzi."

Prof. Mganilwa pia alisema NIT itasaidia sana serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kuongeza idadi ya wataalamu katika miradi mikubwa ya uchukuzi na usafirishaji.

Alisema kuwa chuo kikuu cha usafirishaji ndani yake kutakuwa na vyuo vingine vidogo kama cha Reli na Teknolojia na Uhandisi wa Barabara, Chuo cha Anga, Sayansi na Teknolojia na Chuo cha Uchukuzi na Sayansi.

# Chongolo awaonya wanasiasa wavurugaji

**Na Beatrice Shayo,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema wanasiasa wanaodhani dola au madaraka inaweza kupatikana kwa vurugu, uvunjifu wa amani ama usaliti wajue kuwa haitaweza kwa kuwa serikali zinazoongozwa na chama hicho zipo makini.

Chongolo ameyasema hayo jana wakati akizungumza na wanachama na viongozi wa CCM katika viwanja vya Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui, baada ya mapokezi ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa.

Alisema siku za karibuni kumeibuka kikundi cha wanasiasa waliokataliwa kwenye sanduku la kura na wananchi, ambao wanajipitisha pitisha kila sehemu wakilalama, wakieneza chuki, wakiwakebehi viongozi wa nchi.

"Wanaeneza uongo kwa kujishikiza kwenye masuala wanayoyaita ni matakwa ya wananchi kumbe ni matakwa yao kwani matakwa ya wananchi yalinadiwa na ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/2025 ni vyema wakapumzika maana hawataambulia chochote katika madai yao," alisema Chongolo.

Alisema Watanzania daima wataendelea kukiamini na kukiunga mkono CCM kwa kuwa ndicho kilichobeba dhamana kulinda amani, umoja, mshikamano na maendeleo endelevu.

Kwa mujibu wa Chongolo, kutokana na umuhimu dhamana hiyo, kamwe hakitapoteza muda wa kucheza upatu kwa kuwaunga mkono wasiojua misingi ya nchi na kwa hilo watasubiri sana.

"Wakati wao wakiendelea na siasa zao za kubomoa, sisi CCM tunaendelea na kasi ya kujenga nchi chini ya uongozi imara wa Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi," alisema Chongolo.

Alisema CCM inaridhishwa na namna Rais Samia na Dk. Mwinyi walivyoanza na wanavyoongoza nchi hususani katika kulinda amani, usalama, umoja na mshikamano kwa kuwa ndiyo chachu ya kufanyika kwa maendeleo.

Aidha, aliwataka Watanzania kuendelea kuiunga mkono serikali ili nchi ipige hatua kimaendeleo.

## HABARI MICHEZO

# TREZEGUET: ZIDANE NDIYE ANAMWEZA RONALDO



**PARIS,** Ufaransa

GWIJI wa Juventus, David Trezeguet, amesema hakuna mtu aliyeweza kumnoa vizuri Cristiano Ronaldo kama alivyofanya kocha wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane.


Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, ametumia misimu mitatu iliyopita akicheza pale kwenye dimba la Allianz baada ya kujiunga akitokea Real Madrid kwa ada ya Euro milioni 112.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 36, ambaye amebakiza miezi 12 kwenye mkataba wake, msimu uliopita alimaliza kama kinara wa mabao Serie A akifunga 29.

Amefunga mabao 81 katika mechi 97 za Serie A tangu alipotua hapo Julai mwaka 2018, akishika nafasi ya tatu katika ligi tano kubwa Ulaya nyuma ya Robert Lewandowski (Mabao 93 katika mechi 97 za Bundesliga) na Lionel Messi (mabao 91 katika mechi 102 za LaLiga) kwa kipindi kama hicho.

Na alifunga mabao 311 katika mechi 292 za LaLiga kwa kipindi cha misimu tisa aliyokaa Madrid, ambako alishinda mataji 15, yakiwamo manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ronaldo alitumia misimu miwili kucheza chini ya Zidane pale Santiago Bernabeu, na Trezeguet haamini Massimiliano Allegri, Maurizio Sarri na Andrea Pirlo kama wameweza kumnoa vizuri raia huyo wa Ureno kama ilivyokuwa kwa Zidane.



# *Messi aipagawisha Argentina ikifuzu*

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

KOCHA Mkuu wa Argentina, Lionel Scaloni, amemsifia Lionel Messi kama "mchezaji bora wa wakati wote" baada ya kufunga bao moja na kutengeneza mawili wakati wakishinda 3-0 dhidi ya Equador kwenye robo fainali ya Copa America.

Messi alikuwa mpishi wa ushindi huo wakati 'La Albiceleste' hao wakifuzu hatua ya nusu fainali ya Copa America na sasa watacheza na Colombia kesho Jumanne jijini Brasilia.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or alitengeneza bao la kwanza kwa Rodrigo De Paul aliyefunga dakika ya 40, kabla ya kumtengenezea Lautaro Martinez aliyefunga la pili dakika ya 85.

Messi alifunga la tatu kwa shuti la adhabu ndogo na kufikisha mabao 76 kwa kikosi cha Argentina katika mechi 149 alizoichezea nchi hiyo.

"Ulikuwa mchezo wa Leo, kiukweli sijui kama atachoka kusifiwa kila siku," alisema Scaloni akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Kitu bora ni kwamba, kitu hicho kinatokea kwa sisi tunaopenda mchezo wa soka na katika umri wowote tunaendelea kufurahia."

Ushindi huo ulikuwa ni wa 18 kwa Argentina chini ya Scaloni na sasa wanasubiri kumaliza ukame wa miaka 28 wa kulitwaa taji hilo la Copa America.

# Madrid sasa yamtaka De Beek kwa Varane

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid wameiambia Manchester United kwamba, watamchukua Donny van de Beek mikononi mwao kwa mkopo kama sehemu ya makubaliano ya kumwachia Raphael Varane.

Gazeti la The Sun, limeripoti kuwa Real Madrid pia wanataka kiasi cha Euro milioni 50 kwa ajili ya kumwachia mlinzi huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 28.

Kutokana na Van de Beek kushindwa kupata namba pale Man United tangu asajiliwe kutoka Ajax, hii inaweza kuwa biashara ya kuvutia.

Man United wanajipanga kuelekea msimu mpya huku wakiwa tayari wameshakamilisha dili la mshambuliaji Jadon Sancho kutoka Borussia Dortmund na sasa wanamtaka Varane ili kuimarisha safu yao ya ulinzi.

Lakini Madrid hawataki kumuachia kizembe bila faida, hivyo wanamtaka De Beek kuwa sehemu ya mpango wao huo.

Kwa mujibu wa ripoti, Madrid wanamuona De Beek kama mchezaji mzuri ambaye anaweza kuwa na nafasi ya kutosha kucheza hapo kwenye dimba la Santiago Barnabeu.



HABARI MICHEZO

# Man City kumwachia Jesus wampate Harry Kane

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, ameripotiwa kuwa hana shida kuachana na Gabriel Jesus ili kuongeza nafasi ya timu yake kumchukua, Harry Kane.

Kane anasemekana kuwa ameiambia Tottenham Hotspur juu ya nia yake ya kuondoka klabuni hapo msimu huu wa majira ya joto kusaka mafanikio makubwa zaidi sehemu nyingine.

City wanaaminika kuweka mezani ofa ya kwanza ya pauni milioni 100 kwa nahodha huyo wa England, lakini inasemekana wako tayari kuachana na dili hilo ikiwa Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy, atasimamia msimamo wake wa pauni milioni 150.

Man City wapo tayari kumuacha Jesus aondoke ili waweze kuwa sehemu ya dili hilo la uhamisho wa Kane kutoka Spurs

Biashara ya kubadilishana wachezaji si kipaumbele cha Levy, huku Man City wakiachwa njia panda kufanya maamuzi ambayo yanaweza kuwa kumuuza Jesus mahali pengine kupata fedha za kumnunua Kane.

Kwa mujibu wa Gazzetta dello Sport, Jesus anaweza kuuzwa Juventus ambao wanajiandaa kumuona Cristiano Ronaldo akiondoka, na Guardiola hataweza kumzuia Mbrazil huyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amefunga mabao 82 na kutoa pasi za mwisho 34 katika mechi 195 za City.





# FATI KUANZA MAZOEZI BARCA

**BARCELONA,** Hispania

ANSU Fati ataweza kuanza mazoezi ya mapema ya msimu na Barcelona Julai 12, mwaka huu kama wachezaji wenzake wengine.

Kinda huyo anaendelea kupona vizuri kutokana na jeraha lake la goti ambalo lilimfanya kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu, na kwa idhini ya madaktari wa klabu, atafanya mazoezi kutoka mwanzoni mwa msimu wa mapema.

Lakini, Fati hatatumika haraka kwenye mechi za maandalizi, kwani klabu itahitaji kuwa makini zaidi kuhusu afya yake kwa mujibu wa Marca.

"Kwanza, hatafanya mazoezi pamoja na wachezaji wenzake tangu mwanzo. Fati atafanya mazoezi peke yake mpaka atakaporudi kwa kasi nzuri," ilisema taarifa ya Barcelona kwenda kwa waandishi wa habari.

"Halafu matumaini ni kwamba ataweza kucheza mechi kadhaa za kirafiki kwa nia ya kuwa kwenye kikosi cha mchezo wa kwanza wa LaLiga wa msimu dhidi ya Real Sociedad Agosti 15."

# *Kjaer: Eriksen chanzo mafanikio Denmark*

**LONDON,** England

NAHODHA wa Denmark, Simon Kjaer, amesema tukio la Christian Eriksen katika mechi yao ya kwanza ya makundi ya Euro 2020, liliunganisha kikosi pamoja na kuwasaidia kufika nusu fainali.

Denmark walipata kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Finland katika pambano hilo, ambalo lililazimika kusimama na kuendelea dakika 40 baadaye, baada ya Eriksen kuanguka uwanjani na kuzimia.

Na pia wakapokea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Ubelgiji katika mechi yao iliyofuata. Lakini waliifunga Urusi na kufuzu hatua ya 16-bora, kabla ya kuwafunga Wales 4-0 kufuzu robo fainali.

Akizungumza baada ya ushindi wa 2-1 dhidi ya Jamhuri ya Czech pale Baku juzi, Kjaer alielezea kwamba, Denmark hawataridhika kufika tu hatua hiyo ya nusu fainali.

Alipoulizwa juu ya athari ambayo waliipata kama timu baada ya kuondoka kwa Eriksen ambaye ameondolewa kabisa kwenye mashindano hayo akiwa anajiuguza, alijibu: "Ilibadili jambo kwenye timu.

"Tuko salama pamoja. Tunajua tunaweza kuamini watu walio karibu nasi. Tunajua kwamba ikiwa mmoja wetu ana shida, basi mtu mwingine yuko kwa ajili yake.

"Inatupa usalama na kwa kweli inamfanya Christian ajisikie vizuri sana anapotuona.

"Tunajua kwamba mchezaji aliye karibu nasi yupo na anatuunga mkono."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOUTHGATE ATOA SIRI ENGLAND EURO 2020

●●● Ni wakati akiiwezesha kufuzu nusu fainali baada ya miaka 25 kwa kuifunga...

**ROME,** Italia

KOCHA wa England, Gareth Southgate amesema morali ya kundi zima ya timu yake iliwasaidia kupata nafasi ya kufuzu nusu fainali ya Euro 2020 wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Ukraine, Jumamosi.

**Mabao mawili kutoka kwa Harry Kane na yale ya vichwa yakifungwa na Harry Maguire na Jordan Henderson, yalishuhudia England ikifuzu nusu fainali ya Euro kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 25.**

Na Southgate akapaza sauti yake kuwasifia wachezaji kwa molari na ari waliyoionyesha kwenye mchezo huo na kufanikiwa kusonga mbele.

"Tulionyesha kiwango cha kuvutia sana, si tu wachezaji walioanza, lakini hata wachezaji waliotokea benchi waliendeleza kasi ileile," alisema Southgate akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo uliopigwa katika dimba la Olimpio jijini Rome nchini Italia.

"Kiukweli nafikiria pia kuhusu wachezaji ambao walioondoka dimbani na wale ambao hawakuingia uwanjani.

"Walikuwa sehemu ya mafanikio haya makubwa kwetu. Ni ngumu kundi zima kuweza kuingia uwanjani, lakini walihusika kwa namna nyingine, najisikia furaha na wanajisikia kuthaminiwa.

"Tupo kwenye nusu fainali kwa sababu ya morali. Bila shaka ubora wa mchezo wetu ulikuwa muhimu sana, lakini nimeona mataifa mengi yakitolewa kwa sababu hawakuwa na morali kama vijana wangu."

England sasa itacheza na Denmark kwenye mchezo wa nusu fainali katika dimba la Wembley, Jumatano wiki hii.

Denmark walifuzu nusu fainali hiyo baada ya kuwafunga Jamhuri ya Czech mabao 2-1 katika mchezo wa mapema Jumamosi.

Hii ni mara ya kwanza kwa England kufuzu hatua ya nusu fainali ya michuano ya Ulaya kwa kipindi cha miaka 25.

## ZISIKUPITE

### PSG YAMPA OFA MESSI

KLABU ya Paris St-Germain imetoa ofa ya mkataba kwa mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34, ambaye kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kumaliza muda wake kule Barcelona. Hata hivyo, miamba hao wa La Liga bado wana matumaini ya kumpa mkataba mpya mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or. ***(AS)***

### DE BEEK KUNG'OLEWA UNITED

MANCHESTER United ipo tayari kumuachia Donny van de Beek kuondoka klabuni hapo huku kukiwa na taarifa kwamba anawaniwa na Real Madrid, ambao wanamtaka kiungo huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 24 kwa mkopo. ***(Star)***

### ARSENAL, LIVER KWA SANCHES

LIVERPOOL inataka kumsajili kiungo wa Lille na Ureno, Renato Sanches mwenye umri wa miaka 23, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Arsenal ambao nao wanamtaka nyota huyo wa zamani wa Bayern Munich. ***(Onze Mondial)***

### KROOS KUSTAAFIA MADRID

KIUNGO wa Ujerumani, Toni Kroos, 31, ambaye amestaafu kuichezea timu ya taifa baada ya kutolewa Euro 2020, amesema anatarajia kumaliza kipindi chake cha uchezaji pale Real Madrid. Mchezaji huyo mkataba wake wa sasa na miamba hao wa Hispania unamalizika mwaka 2023. ***(Marca)***

### NIGUEZ ATAKIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inafikiria kumsajili kiungo wa Atletico Madrid, Saul Niguez, 26. ***(La Razon)***

### ARSENAL WAMTAKA JOHNSTONE

ARSENAL wapo tayari kufikiria kumsajili golikipa wa West Brom na England, Sam Johnstone mwenye umri wa miaka 28, kama dili la kumpata nyota wa Sheffield United, Aaron Ramsdale, 23, litashindikana. ***(Star)***

### ALLEGRI AMTAKA POGBA JUVE

KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri, ameitaarifu klabu hiyo juu ya mpango wake wa kutaka kumsajili, Paul Pogba, 28, kutoka Manchester United. Mchezaji huyo mkataba wake Old Trafford utamalizika mwaka 2022, alishinda taji la Serie A akiwa na Juve wakati wa kipindi cha Allegri klabuni hapo. ***(90 Min)***

### SPURS YAMTAKA VLAHOVIC

KLABU ya Tottenham Hotspur inampango wa kumsajili straika wa Fiorentina, Dusan Vlahovic, 21. ***(Corriere dello Sport via Sport Witness)***

### GUENDOUZI HUYO LILLE

KIUNGO wa Arsenal, Matteo Guendouzi, 22, anakaribia kukamilisha usajili wa kutua Marseille. ***(Goal)***

### SOCIEDAD, TAVARES BILABILA

REAL Sociedad imeshindwa katika jaribio lake la kumsajili mlinzi wa kushoto wa Benfica, Nuno Tavares, 21, ambaye anawaniwa pia na Arsenal. ***(Mail)***

## HABARI MICHEZO

# AZAM YASHUSHA KIUNGO MZAMBIA KUTOKA SAUZI

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Azam imeendelea kujiandaa mapema kwa msimu ujao wa Ligi Kuu pamoja na michuano ya kimataifa kwa kufanya usajili wa kiungo mshambuliaji raia wa Zambia, Charles Zulu, kutoka Cape Town City ya Afrika Kusini.

Mtandao rasmi wa kijamii wa klabu hiyo jana mchana umetoa picha ya mchezaji huyo akiwa anapima afya, na baadaye taarifa ikatoka kuwa amefuzu vipimo, hivyo rasmi sasa atajiunga na klabu hiyo kwa mkataba wa miaka miwili.

"Tunayo furaha kuwataarifu kuwa tumefanikiwa kunasa saini ya kiungo mshambuliaji wa kimataifa wa Zambia, Charles Zulu kwa mkataba wa miaka miwili akitokea Cape Town City ya Afrika Kusini. Tumemsajili baada ya kufikia makubaliano na timu hiyo aliyekuwa akiichezea," ilieleza taarifa hiyo kwenye mtandao rasmi wa klabu hiyo.

**Mchezaji huyo ambaye ataanza kuitumikia Azam FC msimu wa 2021/22 kwenye michuano yote ya ligi, kimataifa na mingine, kabla ya kwenda kukipiga Sauzi alikuwa akiitumikia Zanaco FC ya Zambia.**

Zulu anakuwa mchezaji wa pili kusajiliwa na Azam kwa ajili ya msimu ujao baada ya hivi karibuni kumsajili beki wa kushoto aliyekuwa akiwindwa pia na Simba, Edward Manyama, akitokea Ruvu Shooting.

Wakati Manyama anakwenda kupigania namba na Bruce Kwangwa, Zulu atakuwa na kazi ya kuwania nafasi moja na Frank Domayo, Salum Aboubakar na Mudathir Yahaya.

Klabu hiyo yenye maskani yake Chamazi, Dar es Salaam, inadaiwa kuwa kwenye mawindo pia ya kumsajili beki wa kulia wa Coastal Union, Hassan Kibailo.



NI USHINDI TU...

Mashabiki wa Yanga wakichagiza ushindi kwa timu yao wakiwa na kuku na njiwa mweupe kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Simba iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi ambayo waliibuka na ushindi wa bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mauya afunguka alivyoiua Simba SC*

Na Adam Fungamwango

MCHEZAJI wa Yanga aliyefunga bao pekee kwenye mechi ya watani wa jadi dhidi ya Simba, Zawadi Mauya, amesema amefurahi mno kufunga bao hilo, akibainisha kuwa hakupanga na kilichotokea kilikuwa ni ndani ya mchezo tu.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika, alisema ilikuwa mechi nzuri kwao kwa sababu wamepata ushindi ambao tangu awali walidhamiria kufanya hivyo.

"Tumecheza mchezo mzuri. Lile goli sikupanga, ila ilitokea tu. Ulikuja mpira uliookolewa ukawa unazagaazagaa pale na mimi niko karibu nikaukimbilia na kuupiga, lakini kwa sababu tulikuwa na jambo letu, ngoma ikaenda hadi mwisho," alisema Mauya.

Kuhusu mechi ya fainali ya Kombe la FA, alisema kwanza wanaangalia michezo miwili ya mwisho ya Ligi Kuu, hivyo hiyo wanaiweka kwanza kando.

"Pamoja na kuiweka kiporo, lakini pia tumejiandaa kwenda kushinda," alisema.

Beki wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, alisema kipindi cha pili walizuia zaidi kwa sababu ilikuwa ni mipango yao, huku akifurahishwa na ushindi wa timu yake tena mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Naye golikipa wa Yanga aliyefanya kazi kubwa sana, Farouk Shikalo, aliisifu Simba kuwa ni timu nzuri, ndiyo maana wao walijipanga kikamilifu na kuwa makini zaidi hadi kuibuka na ushindi.

"Tumefanya kazi kubwa sana. Simba ni timu kubwa kwa hiyo mimi mwenyewe ilinibidi niwe makini golini, mastraika wao ni hatari ni lazima muda wote uwe kwenye mchezo, kwa hiyo mimi na wenzangu tuliongeza umakini," alisema kipa huyo ambaye ni mara ya pili sasa anacheza 'dabi', ya kwanza ikiwa ni ile ya mabao 2-2, Januari 4 mwaka jana, Ligi Kuu ya msimu uliopita.

## Waziri wa Michezo mgeni rasmi fainali FA

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Tabia Maulid Mwita, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mchezo wa fainali wa Kombe la shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup inayotarajiwa kuchezwa leo katika Uwanja Amaan visiwani hapa.

Mchezo huo unatarajiwa kupigwa majira ya saa 10:00 alasiri ukiwakutanisha bingwa mtetezi wa michuano hiyo, KVZ dhidi ya timu ya Mafunzo.

Timu itakayotwaa ubingwa huo itaiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, CAF.

Akizungumza na gazeti hili Mratibu wa michuano hiyo, Haji Issa Kidali, alisema maandalizi yote kuelekea mchezo huo wa fainali tayari yamekamilika.

Alisema zawadi mbalimbali zitatolewa kwa washindi ikiwamo kombe kwa bingwa pamoja na medali kwa timu wanafainali hao.

## K2GA afunguka ukimya Kings Music

Na Sechellah Nakamba, SJMC

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Karim Zuberi, maarufu kama K2GA, ametoboa siri ya wasanii kutoka 'lebo' ya Kings Music, kutotoa nyimbo mara kwa mara.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, msanii huyo ambaye kwa sasa anatamba na wimbo wa 'Ndombolo', alisema wasanii wote wa kundi lao wamezoea kukaa kimya kwa kuwa hawafanyi kazi kwa kukurupuka.

"Kwanza, nishazoea halafu ninaelewa mipango ya uongozi wetu ipoje. Kwa hiyo, haina haja hata kama tukikaa sana lakini tukitoa nyimbo zinabamba," alitamba.

K2GA pia alifichua siri za bosi wake, Ali Kiba kutoa nyimbo mbili mfululizo, akisema kumetokana na ukubwa wake na uwezo wa kufanya hivyo.

Ali Kiba ameahidi kutoa nyimbo bandika bandua, akitekeleza hilo kwa kuanza na 'Ndombolo' ambao K2GA ameshiriki, kisha siku chache baadaye akaachia 'Salute'.

Kauli hiyo ya K2GA imetoa ishara kwa Kings Music kubadilisha mfumo wao wa kazi, pengine kutokana na lawama zilizoelekezwa kwao na mashabiki kukaa muda mrefu bila kuachia ngoma mpya.

Michezo
Jumatatu Julai 5, 2021
Nipashe



Southgate atoa siri England Euro 2020 UKURASA 22

NI RAHA TU...




Wachezaji wa Yanga wakishangilia baada ya kumalizika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Simba na timu yao kuibuka na ushindi wa bao 1-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nabi atoa siri ushindi Simba, aionya Yanga

● ● ● Asema atairejesha kuwa juu huku akisifu kiwango wapinzani wao, Gomes yeye aahidi furaha...

**Na Saada Akida**

HUKU akitoa siri ya kupata ushindi kwenye mechi ya 'dabi' ya Kariakoo dhidi ya Simba juzi, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amekionya kikosi chake kwamba hakipaswi kubweteka kwa kuwa bado kina kazi kubwa iliyopo mbele yao.

**Yanga ambayo itavaana tena na Simba kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA katika Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma Julai 25, mwaka huu, juzi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya watani zao hao wa jadi katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili, baada ya mchezo huo, Nabi alisema siri kubwa ya kupata ushindi ni baada ya kufanyia kazi ubora na udhaifu wa wapinzani wetu, Simba kabla ya kuikabili.

Alisema aliwasoma Simba vizuri baada ya kucheza nao michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika akiwa Al-Merrikh ya Sudan na kufanikiwa kutumia madhaifu yao baada ya kuangalia ubora wa kikosi cha timu yake.

"Timu zote zilikuwa na mchezo mzuri, na katika mchezo wa leo [juzi], tulitaka kuonyesha jinsi Yanga ilivyokuwa kubwa, kwa upande wangu hii si mara ya kwanza kucheza na Simba, nilikutana nao kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika nikiwa [Al-Merrikh] ya Sudan, pamoja na kupata matokeo haya tusibweteki.

"Simba ina wachezaji wazuri na kocha wake pia, ila nilifanikiwa kusoma mbinu na kupata matokeo mazuri dhidi yao na ushindi huu unaonyesha kiasi gani Yanga ni timu kubwa.

"Mechi hii pia imeonyesha jinsi gani Yanga imerejea licha ya kuwapo kwa changamoto na matatizo kipindi cha nyuma, sasa iko vizuri na nina imani Yanga ile itarejea na kuwa bora zaidi msimu ujao," alisema Nabi.

Alisema Simba ina wachezaji wazuri na wote walikuwapo uwanjani waliwasumbua sana, huku akiwapongeze wachezaji wake kwa kufanya majukumu yao vizuri na kupata ushindi huo.

Wakati Nabi akiyasema hayo, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema matokeo hayo ni mabaya kwa mashabiki na ana imani makosa yao ndio yaliwaadhibu huku Yanga ikiibuka na ushindi huo.

Gomes alisema lawama za mchezo huo atazibeba yeye kwa sababu wachezaji wake walipambana vizuri licha ya kwamba kuna sehemu walikosea na kuadhibiwa.

"Tumepambana vizuri, hatukuwa na bahati ya kupata matokeo, ila inaumiza hasa kuona mashabiki wanapoteza furaha, hivyo tutahakikisha tunaende kujipanga kwa ajili ya mechi yetu ijayo dhidi ya KMC FC ambayo tunahitaji kupata pointi tatu ili kutangaza ubingwa," alisema Gomes.

Alisema wachezaji wake wamepambana kutafuta matokeo, baada ya kutengeneza nafasi nyingi za wazi lakini wakashindwa kuzitumia licha ya kucheza kwa kiwango bora zaidi.

## Madrid sasa yamtaka De Beek kumtoa Varane

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid wameiambia Manchester United kwamba, watamchukua Donny van de...

HABARI UK. 20

## City kumwachia Jesus kwa Kane



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, ameripotiwa kuwa hana shida kuachana...

HABARI UK. 21

9 770856 541002 >